# ZAWADI
# KWA
# GHAZNAWII

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi[as]

**Zawadi kwa Ghaznawii**

Tafsiri ya Kiswahili ya: Tohfa Ghaznawiyya (Kiurdu)

Tohfa Ghaznawiyya (Swahili Translation)

**Mwandishi:**
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

**Mfasiri:**
Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): 1902
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2025

© Islam International Publications Ltd.

**Kwa Maelezo Zaidi:**

**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

**Kenya:**
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

**ISBN:** 978-1-84880-222-3
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

# NENO LA MWENEZI

Mkononi mwenu mna kitabu kingine tena cha Hadhrat Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiya kilichofasiriwa kwa lugha ya Kiswahili chini ya usimamizi wa Dawati la Kiswahili.

Sababu ya kuandika kitabu hiki, Zawadi kwa Ghaznawii, kilikuwa ni kwamba mtu mmoja Maulawii Abdul Hak Ghaznawii alitoa kipeperushi alimomshabulia Seyidna Ahmad[as] kwa mdomo mchafu na kufanya masihara na dhihaka – jambo ambalo ni kinyume na mwenendo wa muungwana yeyote. Seyidna Ahmad[as] amemjibu ndani ya kitabu hiki barabara mpaka kufumba mdomo wake.

Habari ya mubahala nayo imetajwa humu ndani iliyofanyika na Maulawii Abdul Hak, ambao baada yake Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ilipata maendeleo makubwa. Maelezo yake tosha pia yameandikwa humu ndani.

Maulawii Abdul Hak Ghaznawii alikuwa ni mwanafunzi wa mja mwema mmoja marehemu Maulawii Abdullah Ghaznawii aliyesema kabla Seyidna Ahmad[as] alikuwa hajatumwa na Allah maneno ya bishara kwamba: ‘Nuru moja imeshuka kutoka mbinguni, naye ndiye Mirza Ghulam Ahmad Qadiani!

Pia akawasomea watu kashfi yake: 'Nuru moja ikaanguka na ikateremkia Qadian, lakini kizazi changu kikanyimwa hiyo.'

Mfasiri wa kitabu hiki ni Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani. Twamshukuru kwa juhudi yake kubwa. Kabla ya kupeleka mtamboni, nikaisoma kwa uangalifu na kulinganisha na matini ya Kiurdu na kurekebisha ili kuisogeza karibu zaidi na lugha chanzi.

Ingawaje Kitabu kiliandkiwa mwaka 1900, lakini kikachapwa na kuenezwa Oktoba 1902.

Sheikh Ansar Hussain anastahili kushukuriwa; yeye ndiye aliyepanga herufu hizi kwa kompyuta na kutayarisha fomati.

Mola Mtukufu Awajalie wasomaji kujinufaisha ipasavyo. Amin.

Jamil R. Rafiq

Wakilut-Tasnif

Tahrike Jadid

Rabwah, Pakistan 10 Septemba 2023

ٹائٹل بار اول

الحمد للہ
والمنۃ کہ رسالہ ہذا
از تصنیفات حضرت
امام ہمام مسیح موعود و مہدی معہود
جناب مرزا غلام احمد صاحب نصرہ اللہ وایدہ
الموسوم بہ

# تحفہ غزنویہ

سنہ ۱۹۰۲ء
بماہ اکتوبر

مطبع ضیاء الاسلام قادیان ضلع
گورداسپور میں باہتمام حکیم حافظ
فضل الدین صاحب
بھیروی مالک مطبع
چھپکر شائع
ہوا

قیمت ۴ر — محصولڈاک ار — وی پی ار — کل ۶ر

تعداد اشاعت
۷۰۰

Jalada la chapa ya kwanza

Ni sifa njema za Allah na hisani Yake kwamba miongoni mwa vitabu vilivyo-andikwa na Hadhrat Imamu Mtukufu Masihi Mau‘udi na Mahdi Mau‘udi Janabi Mirza Ghulam Ahmad – Mungu Amsaidie na kumwauni – kijitabu hiki kiitwacho

# ZAWADI KWA GHAZANAWII

## Oktoba 1902

kimechapishwa katika Matbaa Dhia-ul-Islam, Qadian, Wilaya ya Gurdaspur, chini ya usimamizi wa Hakiim Hafidh Fadhl-ud-din wa Bhera, mwenye matbaa.

Bei: Anna 4

Gharama ya Posta: Anna 1

Vp: Anna 1

Jumla: Anna 6

Nakala 700

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ [1]

نحمدہٗ ونصلّی [2]

# Jibu la Tangazo la Abdul Hak Ghaznawii

☆

**[Shairi la Kiajem]:**

Ewe, uliyejiandaa kunidhalilisha, na huna kazi nyingine isipokuwa kunilaumu,

kila wakati unafumbua mdomo wako dhidi yangu, mbona humwogopi Mungu Mjuzi wa mambo ya gaibu.

Yapasa kujadiliana kwa takwa; ewe mvovu, mpaka lini utaendelea kunitusi.

Wewe si mbwamwitu a pori wala nyoka; acha tabia hii, na uone haya mbele ya Mungu.

Ewe mwenye hasira, nashangaa kwa sera yako kwamba huna habari ya uhakika, u mtovu wa adabu.

Simama ukarekebishe kwanza ufahamu wako; yapasa jicho la mkinzani liwe sawa.

Mdomo mchafu huufanya moyo kuwa mweusi, wenye mdomo mchafu hawapati kumkurubia Mungu.

---

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

[2] Twamhimidi Yeye na kumsalia Mtume.

Usikae na wafanyao masihara ili ujumuike na waongofu.

Kazi yako usiku na mchana ni kunilaumu, kuapiza na kuhakirisha imekuwa ndiyo kazi yako.

Laana ndiyo ile inayokuwa kutoka kwa Rahmani; laana ya mtu asiyefaa na duni haina ukhakika wowote.

Kama mjinga akitulaani, hiyo haituangukii, bali anajifedhehesha mwenywe.

Aliye mnyofu, kwa nini ashangae juu ya kazi ya Mungu.

Mungu Amuumbaye binadamu kwa tone moja tu, na kwa magao mawili ya begu hutegeneza bustani,

Kama Akimfanya mtu kama mimi kuwa Masihi, au akimfanya maskini kuwa mfalme,

Basi jambo hili si mbali na fadhili na ukarimu wake. Yu kipofu aliyelikataa hili.

Naam, usikate tamaa na Yule Mtukufu, uwe mtumishi mwaminifu kisha jichukulie utakacho.

Yu Mola Mweza, Mwumbaji, Mtukufu; Hufanya Apendacho, nani ameona unyonge Wake.

Huumba uso mwangavu kwa tone la manii na Hulifanya jiwe kuwa rubi.

Anapomfanyia mtu ukarimu, Humfanya mtu wa ardhini kuwa mtu wa mbinguni.

Hivyo ndivyo Alivyonifanyia ukarimu na kunijalia fadhili nyingi.

Mimi mwenyewe nikawa dhihirisho la Yule Asiye na mfano, na nikawazidi wote katika ujuzi na maarifa.

Mungu wangu Ananifanyia sana wema, ninazo mamia ya ishara, kama mtu akija kuziona.

Enyi wafu, sikilizeni, ni mzima mie; na enyi mausiku yenye giza, mimi ninang'aa.

Macho yangu haya mawili yapampayo kichwa change, yamwona Rafiki Aliye Rafiki yangu mpendwa.

Mguu wangu unaifikia Arshi ya Mungu, na masikio yangu haya mawili yanapata habari kutoka kwa Mungu.

Nimejaaliwa malaki ya neema, na uso wangu huu wamefichiwa wengine.

Wakati wote nawaonyesha wenye sifa ya Firauni mamia ya ishara zilizo aina ya mkono mweupe wa Musa.

Wenye tabia mbovu ni vipofu na viziwi kwa kuona ishara hizi, hawajali hata kwa kuona mamia ya ishara.

Nipo mbali na macho ya watu; hajui yeyote daraja yangu.

Walishindana nami kwa kupungukiwa akili, na wakanyimwa kunikubali wakiwa wenye bahati mbaya.

Hakuna ajuaye siri ya batini yangu akili yao haifikii mlangoni pangu.

Jazba yao na vita yao ni kwa sababu ya ujinga, na kuzima nuru ya Mungu ni kusudio lao.

Ewe uliyedanganyika, ukija kwetu na kuwa mwaminifu, na kukaa nasi kwa muda ukiwa mkweli na kwa nia ya kutafuata haki,

Basi utaona 'ulimwengu' wa ishara za Mungu, zinazokuja kuvutia dunia kwenye Mungu.

Sitaki kukusumbua kuhusu habari hii, niko tayari kukupa dinari moja kila mwezi (kwa posho yako).

Yapasa kukaa kwangu kwa mwaka mmoja; kutoka kwangu hii ni ahadi na kutoka kwako kufuata sharti ni lazima.

Kama mwaka huu wa ahadi yangu ukipita bila kudhihiri ishara yoyote, waweza baada yake kusema uyatakayo kusema.

Hii hii ndiyo njia ya watu wema na suna yao, njia ya haraka ndiyo njia ya laana.

Mtu ambaye batini yake imeng'aa kutoka kwa Mungu, kukaa naye hata kwa muda mfupi sasa pia humfanya kuwa 'dhahabu'.

Kwa mtu anayezingirwa na giza, kufungamana na watu wema ni mwombezi.

Mungu Hufanya urafiki na marafiki zake, na Huwasaidia waaminifu.

Mtu anayeingiwa na upendo Wake rohoni na moyoni mwake, mara imani yake hupata kuhuika.

Upendo wa Mungu hudhihiri usoni pake, na mnukio wake husikika kutoka nyumbani mwake na mtaani mwake.

Kumzuru yeye ndiyo kama kumwona Mungu; na Mwenyezi Mungu Huwa Anamsaidia.

Mwenyezi Mungu Huonyesha kazi nyingi kubwa kubwa duniani humu kwa ajili ya heshima yake.

Humjalia mamia ya mionzi kama jua, ili nafsi yeyote apate kuokoka katika mapazia ya giza.

Mwenyezi Mungu Amenifanyia ukarimu mwingi, wanikataao wajidhulumu wenyewe.

Elimu ya Kurani, elimu ya lugha ile takatifu na elimu ya ghaibu kwa Wahyi wa Mungu –

Elimu hizi tatu nimejaliwa kama ishara, na zote tatu zimesimama kama mashahidi kwa kuniunga mkono.

Hakuna mtu awezaye kunikabili katika uwanja huu.

Hoja imewakamilikia kutoka kwa Rahmani, watu wasiofaa wamebakiwa na kupayuka tu.

Wakati wa jua na mwezi kupatwa mwezi na jua pia vikaanguka mbele yangu kwa kukosa nuru zao.

Rahmani Akaonyesha ishara hii huko mbinguni, na ardhini pia Akaonyesha mkono wake wa kuogofya.

Rafiki yangu Yu Mkarimu kwangu; Yeye Akawa wangu, nami nikawa Wake.

Mpendwa wangu Akaingia rohoni, akilini na ngozini mwangu; furaha yangu ndiyo kumkumbuka Yeye.

Zipo siri kadhaa kati yangu mimi na mpendwa wangu, na adhama Yake hudhihirika kwa njia yangu.

Kila mmoja anashikamana na mtu yeyote, lakini sisi tumeshikamana na Mungu Aliye Mwenye uzima, Mhifadhi na wa Pekee.

Ni masikitiko kwamba watu wangu hawakunitambua, na wakapoteza imani yao kwa husuda.

Dunia hii dhalimu ni kipofu na kizivi na macho yake ni mabovu zaidi kuliko macho ya bundi.

Nilipokuwa chembe waliniheshimu, lakini wakati ambapo nikawa jua wakanidharau.

Mian Abdul Hak Ghaznawii ametoa tangazo moja linaloonekana kwa hakika kutoka kwa Sheikh Abdul Jabbar na nduguze. Mungu ndiye Ajuaye zaidi. Katika tangazo hili kadiri ulivyotumika ukali, mzaha na masihara, iliyo njia ya majahili tangu zamani, tukimwachia Mwenyezi Mungu uadilifu wake, twajibu mambo ya msingi, kwa kujaliwa na Mwenyezi Mungu.

Tangazo hilo linabeba mashambulizi ya aina mbili. Kwanza, Mian Abdul Hak akitaja baadhi ya ishara na bishara za zamani zilizoishatimia kwa hakika au ziko karibu kutimia, akataka kuwahadaa watu wa kawaida kwamba hazijatimia. Kwa mfano, anaandika katika tangzao lake kwamba bishara kuhusu Deputy Atham, Ahmad Beg wa Hoshiarpur na mkwewe hazijatimia. Lakini, nashangaa kwamba baada ya kuitwa masheikh, roho ya hao watu inakubalije kusema uongo mchafu kama huo; nani asiyejua kwamba bishara hizi mbili zilikuwa na sharti la kurejea kwenye haki na kutubu. Lakini, Ahmad Beg, kwa vile hakuwa na mfano wowote wa kutishia mbele ya macho yake, hakuweza kujifaidisha na sharti hili na akafa sawa na lengo la bishara barabara katika miadi, na kifo chake kilitimiza sehemu moja ya bishara. Ahmad Beg alikuwa mtu ambaye kifo chake kiliwaombolezesha Masheikh wapinzani. Na Sheikh Muhammad Husain akaandika, 'Kwa yakini mtu huyu anajua elimu ya unajimu ambaye bishara yake imetimia

waziwazi hivyo.' Lakini mkwe wa Ahmad Beg na wazazi wake na jamaa zake walipoona kwa macho yao mfano huu wa kutisha, wakatawaliwa na hofu kiasi hiki kwamba alichukuliwa kama mfu kabla ya kufa. Kwa hiyo, kama ilivyo tabia ya kibinadamu, kwa kushuhudia hiyo, moyoni mwao mkazalika hali ya kurejea kwa Mungu. Na baadhi yao wakaniandikia barua kuwasamehe kosa lao. Katika nyumba zao vilio vikaanza usiku na mchana na wakajishughulisha kutoa sadaka, kusali na kufunga saumu, na watu wa kijiji hiki waliendelea kusikiliza vilio, kelele za wanawake. Ilmuradi, wanawake kwa wanaume wote walijaa hofu, na sawa na kaumu ya Yunus[as], kwa kuona adhabu wakshughulikia kutubu, na kutoa sadaka. Sasa tafakarini, katika hali hii Mwenyezi Mungu Angewatendea namna gani. Kadhalika Deputy Atham pia alikwishapata kusikiliza matokeo ya ishara kuhusu Ahmad Beg, na kupitia magazeti na vipeperushi, ishara hii ikajulikana kwa malaki ya watu. Kwa hiyo, yeye naye baada ya kusikiliza utabiri akadhihirisha athari za hofu na kutishika. Kwa hiyo, sawa na sharti la utabiri, Mwenyezi Mungu Akaahirisha adhabu, kwani sharti lile lilikuwa ni ahadi ya Mungu naye Havunji ahadi yake. Swala hili limekubalika na watu wote, Waislamu, Wakristo na Wayahudi, wote wameafikiana juu ya itikadi hii kwamba onyo, yaani utabiri wa adhabu unaweza kuahirishwa

hata bila sharti la kutubu, kustaghafiru, na kuhofia, kama bishara ya Nabii Yunus[as] yenye miadi ya siku arobaini isiyokuwa na sharti lolote ikafutika, na wakazi wa Ninawi waliokuwa zaidi ya laki moja, hata mtoto mmoja miongoni mwao hakufa, na Nabii Yunus[as] kwa kufikiri na kujuta kwamba bishara yake imebatilika, akatoroka nchini. Sasa, tafakarini kwamba je huu ni uaminifu kwamba wakti wa kuleta upinzani huu hawakumbuki habari hiyo. Na hapo pana maneno haya ya Hadihi: قَالَ لَنْ اَرْجِعَ اِلَيْهِمْ كَذَّابًا yaani Yunus[as] akasema, sasa nikiitwa kadhabu, sitarejea kamwe kwa watu hao. Kama mnaamini Hadithi basi tazameni Hadithi katika Durri Manthuur katika maelezo ya sehemu hiyo. Na kama mnaamini Biblia ya Wakristo, basi someni kitabu cha Yona Nabii. Kwa vyovyote yafaa kuona haya wakati fulani. Utovu wa haya na imani haviwezi kujumuika. Mtamjibuje Mwenyezi Mungu kuhusu jeuri na dhulumu hii kwamba mlishuhudia bishara mia zikitimia kwa uwazi lakini hamkujifaidisha nazo, na bishara moja au mbili msizozifahamu kwa ujinga wenu zilizokuwa na masharti, mkazipigia makelele. Lakini makelele haya hayahusikani nami tu na bishara zangu. Ebu, tajeni jina la Nabii yeyote ambaye kuhusu baadhi ya bishara zake ambazo wapumbavu hawakupiga kelele kwamba hazikutimia. Nimeshaandika hivi punde kwamba maonyo yaani kuhusu bishara ya adhabu, ni suna hii tu

ya Mwenyezi Mungu kwamba liwepo sharti kwa bishara au la, yeye Huahirisha kwa sababu ya kujinyenyekeza, kutubu na kuhofia. Kuhusu jambo hili, si kisa cha Yunus[as] tu kinachoshuhudia, bali kutokana na Kurani, Hadithi na Vitabu vya Manabii wote yathibitika kwamba Mwenyezi Mungu Anaponuia kumwadhibu mtu na kutaka kumshushia balaa, basi balaa hiyo yaweza kuahirishwa kwa kuomba, kutubu na kutoa sadaka. Sasa ni dhahiri kwamba ile adhabu Anayonuia Mwenyezi Mungu kutoa, kama Akimjulisha kuhusu nia yake Nabii au Mtume au Muhadathi, basi nia hiyo inaitwa bishara. Basi, ilipokubaliwa kwamba nia ile inaweza kuahirishwa kwa dua, sadaka na kufanya mambo ya heri, basi kuna sababu gani nia hiyo isiweze kuahirishwa kwa sababu tu mpokeaji wahyi fulani amepashwa habari yake. Je, nia ile hugeuka kuwa kitu kingine baada ya kupasha habari? Au baada ya kupasha habari, Mungu Anaona vigumu kuiahirisha kwa dua, toba na sadaka, lakini kabla ya kupasha habari Haioni vigumu? Ni masikitiko kwamba wasioelimika hawaoni tofauti kati ya ahadi ya Mwenyezi Mungu na onyo lake. Katika onyo, kwa kweli, haiwi ahadi, inakuwa hii tu kwamba Mwenyezi Mungu kwa utukufu wake Anataka kumwadhibu mkosefu na baadhi ya wakati Humpasha pia mpokeaji wahyi kuhusu matakwa yake. Lakini, mkosefu huyo anapotimiza mapasiko ya matakwa yake kutubu, kustaghafiru,

unyenyekevu na vilio, hapo rehema ya Mungu inashinda ghadhabu Yake na huficha na kusitiri ndani mwake ghadhabu. Hiyo ndiyo maana ya aya hii عَذَابِیۡۤ اُصِیۡبُ بِہٖ مَنۡ اَشَآءُ ۚ وَ رَحۡمَتِیۡ وَسِعَتۡ کُلَّ شَیۡءٍ[3]. Yaani rehema Yangu imeishinda ghadhabu Yangu. Isipokubaliwa kununi hii, sheria zote zabatilika. Basi, masikitiko makubwa yalioje juu ya wapinzani wetu kwamba wanapinga hata sheria ya Kiislamu kwa sabau ya kunichukia. Wanaposikia jambo la haki hawatumii takwa, bali wanatafakari namna ya kulipinga kwa njia yoyote. Haijulikani watafikia mpaka wapi wakiendelea kupinga maarifa ya kweli. Hii iliyoandikwa kwamba kwa kukabiliana na mawalii hutia imani hatarini. Hatari hiyo hutokea kwa sababu hii pia kwamba kauli za Masidiki na Mawalii zatoka katika chemchemi ya ukweli na huwa nguzo ya imani, lakini mpingaji wao anajiwekea kanuni ya kuendelea kupinga kila kauli yao, asikubali yoyote. Kwa kuwa husuda na uadui ni balaa mbaya, hivyo siku moja anapata kupinga jambo linalofutilia mbali imani yake mara moja. Mathalani, masiala haya kwamba nia ya Mungu ya kuadhibu, hata kama Amemdhihirishia mpokeaji wahyi nia ile au la, inaweza kuahirishwa kwa dua, sadaka, toba na kuomba msamaha, ni kweli kabisa, ni kiini cha sheria na waliyoafikiana nayo Manabii wote. Lakini, je yawezekana mtu atiiye nafsi aliye mpinzani wangu

[3] Al-A‘raaf 7:157

atakubali jambo hili la maarifa akilisikia kutoka kinywani mwangu? La hasha. Huyo akisikia tu mara ataanza kutafuta mbinu ya kulipinga ili kusababisha kukadhibisha bishara yoyote. Kama mtu huyu angekuwa na hofu ya Mungu asingewajali watu wala asingekuwa na shabaha ya kujionyesha, bali angefahamu amesimama mbele ya Mungu na angesema yaliyostahili kusemwa kwa kuzingatia takwa, na angekabili kulaumiwa na kulaaniwa na watu, lakini angetoa ushahidi wa ukweli. وَلٰكِنْ اِذَا غَلَبَتِ الشِّقْوَةُ فَاَيْنَ السَّعَادَةُ [Lakini bahati mbaya inapotawala, bahati njema i wapi?]

Upinzani wa pili wa Mian Abdul Hak ni huu kwamba pendekezo nililotoa kwa ufunuo wa Mwenyezi Mungu kama kutimiza hoja, ambalo nilichapisha kwa njia ya tangazo hapo kabla pia, yaani shindano la dua kukubaliwa kwa njia ya kuwaponya wagonjwa. Mian Abdul Hak hakubali pendekezo hili na anatoa udhuru kwamba masheikh na maulamaa wote wa India na Panjab wajumuikeje, na nani atoe matumizi yao. Lakini ni dhahiri kwamba huu ni udhuru mbovu na wa kipuuzi. Katika hali watu hao hula maelfu ya rupia za kaumu, ni shida gani kutoa rupia 2-4 za nauli kwa kazi muhimu ya namna hii. Tumekubali kwamba watu hao hawawezi kuvumilia shida yoyote kwa ajili ya dini, lakini kwa jambo muhimu kama hili kwamba maelfu ya watu hutoka katika kucha zao na wanaendelea kuwa makafiri

sawa na maoni yao, kutoa dirhamu chache kwa nauli si shida kubwa. Na kama yupo mtu ambaye hali yake inaafikiana na ضُرِبَتۡ عَلَيۡهِمُ الذِّلَّةُ[4] , basi hana haja ya uwakili wa Abdul Hak; mimi naweza kumlipia nauli ya safari mpaka ***kos***[5] mia mbili. Huyo akiazimia pesa afike Lahore, na anionyeshe cheti cha chifu yeyote wa mji wake kwamba kwa kweli huyu Sheikh au Pirzada amebanwa sana na umaskini, ameazima fedha na amefika Lahore. Basi, naahidi kulipa nauli ile, sharti asiwe Sheikh au Pirzada wa jina tu, bali awe anajulikana kama vile Nadhiir Husain wa Delhi na kadhalika. Na kama pendekezo hili halikubaliki, basi maulamaa na masheikh wa vilaya ya Lahore, Amritsar, Gurdaspur na Ludhiana tu wajumuike. Miongoni mwao pia kwa sharti lililotajwa juu nitalipia nauli ya kila mwenye shida. وَإِنۡ لَّمۡ تَفۡعَلُوۡا وَلَنۡ تَفۡعَلُوۡا فَاعۡلَمُوۡٓا اَنَّكُمۡ سَتُرۡجَعُوۡنَ اِلَى اللّٰهِ ثُمَّ تُسۡـَٔلُوۡنَ.[6]

Kisha, Mian Abdul Hak baada ya kutoa udhuru tuliojibu sasa hivi, ameomba kimasihara na kidhihaka na katika masihara haya hakubaki nyuma kuliko wakataaji wa zamani. Kwani, Waarabu hawakuomba kamwe kidhihaka na kimasihara ishara za namna hii kwamba

[4] Aali 'Imraan 3:113

[5] *Kos* moja na kama maili mbili. Mwenezi.

[6] Tafsiri: Na msipofanya, na hamtafanya kamwe, basi jueni mtarejeshwa kwa Allah, kisha mtaulizwa.

mguu wenye kasoro wa shabaha fulani urekebike au mtu asiye na nguvu ya kuona apone. Naam, watu wa Makka waliomba ishara hii kwamba nyumba ya Mtume Mtukufu[saw] igeuke kuwa ya dhahabu, mito ikitiririka, pembezoni mwake; na pia kwamba yeye apande mbinguni mbele ya macho yao na ashuke kutoka mbinguni mbele ya macho yao, na alete pamoja naye Kitabu cha Mungu ambacho wakikishika mkononi wakikague pia, ndipo wataamini. Ingawaje ombi hilo lilikuwa la kijinga lakini haliikuwa na sharti ya kuudhi kama ombi la Mian Abdul Hak. Kadhalika, watu walimwomba Hadhrat Isa[as] ishara. Lakini ni dhahiri kwamba waombaji hawakupewa ishara walizoomba, bali wakajibiwa kwa kukaripiwa na kukemewa. Na katika Kurani Tukufu waombaji ishara za kuombwa wakajibiwa kwamba قُلْ سُبْحَانَ رَبِّيْ هَلْ كُنْتُ اِلَّا بَشَرًا رَّسُوْلًا[7] . Yaani adhama ya Mwenyezi Mungu ni mbali sana na jambo hili kwamba Mtume au Nabii au Mpokeaji wahyi yeyote aweze kuonyesha kwa nguvu yake mambo ya kimuujiza yauhusuyo Uungu. Na Akasema, waambie mimi ni Mtume tu mmoja miongoni mwa wanadamu nisiye na madaraka ya kufanya kazi yoyote mwenyewe, nafuata tu amri ya Mungu. Hivyo, kuniomba nionyeshe ishara hii, na nisionyeshe hii, ni ujinga kabisa. Naweza kuonyesha

[7] Banii Israaiil 17:94

yale tu Aliyosema Mwenyezi Mungu siyo mengine. Na katika Injili, Hadhrat Maishi[as] aliwaambia waziwazi waombaji ishara ya kubuniwa kwamba kizazi cha zinaa chaniomba ishara, lakini hakitapewa ishara isipokuwa ile ishara ya Nabii Yona. Yaani, ishara itakuwa ni kwamba licha ya juhudi sana ya maadui ya kutaka kunihilikisha msalabani, mimi, kama Nabii Yunus, nitaingia mzima katika tumbo la kaburi lifananalo na samaki, na nitatoka humo mzima, kisha kama Nabii Yunus[as] nikisalimika nitahamia nchi nyingine. Hii iliashiria kwenye tukio lile alilotoa Mtume[saw] wa Allah habari yake jinsi inavyothibitika katika Hadithi iliyomo katika *Kanzul Ummaal*, yaani hii kwamba Isa[as] akiokoka msalambani akakimbilia nchi baridi , yaani Kashmir, ambayo katika mji wake Srinagar lipo kaburi lake. Ilmuradi, maadui walipomuomba Hadhrat Masihi[as] ishara na kama Mian Abdul Hak wakataka baadhi ya ishara za kubuniwa kwamba tuonyeshe hii na hii, ndipo Hadhrat Isa[as] akawajibu jinsi tulivyoandika sasa hivi. Hii yaonyesha kwamba Mian Abdul Hak hakukosea katika kuomba ishara za kubuniwa, bali sawa na aya تَشَابَهَتْ قُلُوْبُهُمْ[8] , asili yao inafana na makafiri wenye bahati mbaya ambao hawakukubali ishara za Mwenyezi Mungu, bali wenyewe wakibuni walikuwa wakiomba kwamba onyesha ishara

[8] Al-Baqara 2:119

kama hizi. Lakini, masikitiko ni haya tu kwamba watu hao licha ya kuitwa masheikh, wanafuata desturi ya masihara na dhihaka. Atakayesoma kwa makini kipeperushi cha Abdul Hak, atalazimika kukubali kwamba akitaja ndugu yetu Maulawii Abdul Karim kwa shari na utovu wa adabu, ishara aliyotaka ya kurekebisha mguu wake au kuhusu macho yake, ndiyo masihara aliyofanya kwa njia chafu ambayo siyo kazi ya mtu mnyofu na mwema. Mambo machafu hutoka katika moyo mchafu na mambo mema hutoka katika moyo mwema. Mtu hujulikana kutokana na kauli zake jinsi mti hujulikana kwa matunda yake. Ikiwa Mwenyezi Mungu Alisema katika Kurani Tukufu لَا تَنَابَزُوْا بِالْاَلْقَابِ[9], yaani msiwaite watu kwa majina yanavyowachukiza, kisha kutenda kinyume cha aya hii ni kazi ya akina nani. Lakini, sasa hatumsikitii Abdul Hak wala marafiki zake, kwani dhuluma, jeuri uongo na uzushi vimepita mipaka. Kisomeni kipeperushi hicho hicho kwamba ametumia uongo sana kiasi gani. Je ameona, sehemu, yoyote haya mbele ya Mwenyezi Mungu? Basi, kwa mfano tu twaandika hapa chini rundo la uongo wa huyu mdhalimu, kwa njia ya 'Kauli yake' na 'Nasema', aliotumia katika kipeperushi hicho, nao ni huu:

[9] Al-Hujuraat 49:12

**Kauli yake**: Mirza mara nyinig aliaibika katika mijadala ya sehemu mbali mbali, akawa hana la kujibu, na katika kila hafla akashindwa na hakupata muradi.

**Nasema**: Ebu Mian Abdul Hak, je hii umesema kweli? Je, hata sasa tusiseme: لَعْنَةُ اللهِ عَلَى الْكَاذِبِيْنَ [Laana ya Mungu iwe juu ya waongo]. Shabashi, umeonyesha vizuri sana mfano wa Abdallah Ghaznawii. Wanafunzi wapasa wawe hivyo. Kama u mkweli, basi eleza vizuri zile hafla na vikao nilimoaibika. Mbona unaongopa sana hivyo. Je, hutakufa? Ebu, andika ibara za mijadala ambako wewe au ndugu yako mwingine alishinda, waila si mimi tu bali hata mbingu pia yasema لَعْنَةُ اللهِ عَلَى الْكَاذِبِيْنَ [Laana ya Mungu iwe juu ya waongo]. Kwa upande wangu ingewezaje hoja kutimizwa zaidi ya hii kwamba nikathibitisha kwa Kurani kwamba Hadhrat Masihi[as] ameshakufa. Nikathibitisha kwa Hadithi kwamba Hadhrat Masihi[as] ameshafariki na umri wake ulikuwa miaka mia na ishirini na mitano. Hadithi ya Mi'raji imethibitisha kwamba akaenda kuungana na wafu, na Nabii wetu[saw] alimwona kwenye mbingu wa pili pamoja na Hadhrat Yahya[as]. Je bado imebaki kasoro katika kufa kwake. Masahaba wote wakaafikiana juu ya kifo chake. Kama ijima haikufanyika, basi eleza kuhusu mawazo ya Umar[ra] yasiyo sahihi kwamba Mtume Mtukufu[saw] hakufa na atarudi tena duniani, Hadhrat Abu Bakr[ra] alipotoa

aya hii مَا مُحَمَّدٌ اِلَّا رَسُوۡلٌ ۚ قَدۡ خَلَتۡ مِنۡ قَبۡلِهِ الرُّسُلُ[10] , basi akatoa aya hii kwa kufahamu nini na alikuwa na shabaha ya kuthibitisha nini iliyoafikiana na hali ile na Mashaba wakaelewa maana gani na kwa nini hawakupinga, na kwa nini imeandikwa sehemu hiyo kwamba Masahaba waliposikia aya hii mara wakaachana na mawazo yao. Kadhalika, nimeshathibitisha kutokana na Hadithi kwamba Masihi Mau'udi ajaye atatokana na umati huu huu, na zama za kudhihirika kwake ni hizi kama yafahamika kutokana na Hadithi يَكْسِرُ الصَّلِيْبَ [Atavunja msalaba]. Tena fumbua macho na tazama kwamba wakati wa mwito wangu, jua na mwezi zilipatwa huko mbinguni katika Ramadhani sawa na Hadithi, na kwa mkono wangu karibu ishara mia zilidhihirika ambazo lukuki za watu ni mashahahidi wake, ambazo maelezo yake yameandikwa katika kitabu *Tiryakul Kuluub*. Haikubaki njia yoyote ambayo kwayo sijatimiza hoja. Kimaandiko nilitimiza hoja, kiakili nilitimiza hoja, kwa ishara za mbinguni nilitimiza hoja. Sasa kama una haya, basi tafakari mwenyewe kwamba nani aliaibika na kushindwa na kukosa kupata muradi wake. Sikuishia hapo tu, mara kadhaa nilitoa matangazo kwamba kama mnao ukweli kiasi chochote, basi njooni kushindana nami. Onyesheni katika Kurani au onyesheni katika

[10] Aali 'Imraan 3:145

Hadithi, imeandikwa wapi kwamba Hadhrat Isa[as] alikwenda mbinguni mzima na mwili wake na kisha atashuka mzima na mwili wake kutoka mbinguni. Hata sasa pia niko tayari kukubali kama mnaweza kuthibitisha sawa na Hadithi maana ya aya hii فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي[11] kuwa minghairi ya kufisha na kuhilikisha, au kwa aya au Hadithi yoyote kupanda mbinguni kwa Hadhrat Isa[as] na mwili au kushuka kutoka mbinguni na mwili. Au kama katika habari za ghaibu zinazodhihirika kwangu kutoka kwa Mwenyezi Mungu muweze kushindana nami, au katika kukubaliwa dua muweze kukabiliana nami, au katika kuandika lugha ya Kiarabu muweze kushindana nami, au katika ishara za mbinguni nilizozipewa muweze kushindana nami, basi nitakuwa mwongo. Mkawa kama wafu wakati wa maswali haya. Hiyo ni sababu kwamba kwa kutengana nanyi, maelfu ya watu wema na maulamaa wanaendelea kujiunga na Jumuiya hii. Ee azizi, maneno hayo maovu ya kipuuzi hayawezi kufaa kitu. Je, watafutao haki waweza kuzuilika na mambo ya kipuuzi kama hayo? Huu sio mji wa Ghazni, bali ni Panjab ambako kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu siku hadi siku watu wanazidi katika akili na busara. Na nimeona kwamba kwa sababu ya kauli chafu hizo za uwongo, watu wenye akili wanaendelea kukosa imani

[11] Al-Maaida 5:118

juu yenu kiasi hiki kwamba ingawa sasa watu mahususi wenye elimu na wenye jaha na mali wapo karibu elfu kumi katika Jumuiya yetu, lakini idadi kwa jumla ni zaidi ya hata elfu thelathini. Sababu yake i nini? Ni hii tu kwamba mnatumia masihara, dhihaka na matusi tu kupata shabaha yenu, hamfuati njia ya unyofu. Ilikuwa ni rahisi kwamba mnaitwa wapokeaji ufunuo na pia mnayo madai ya kupokelewa maombi, basi zichapisheni kwa njia ya kipeperushi bishara chache kuhusu kukubaliwa kwa maombi, na kwa upande wangu mimi pia nizichapishe, na muda usiwe zaidi ya mwaka mmoja. Kisha ikiwa bishara zenu zikitimia, basi mara moja maelfu ya watu wa Jumuiya yangu watajiunga nanyi na mwongo atadhalilika. Je, mtakubali ombi hili? Haiyumkiniki. Basi, hiyo ndiyo sababu kwamba watafutao haki wanaendelea kuchoka nanyi. Nani ataamini kwa sababu tu ya matusi na uzushi pasipo uthibitisho. Sasa pia nikiwahurumieni nimechapisha tangazo moja, na tangazo moja limechapishwa na Jumuiya yangu, lakini je ni yumkini mtaweza kuhudhuria kwa uamuzi katika mkusanyiko wowote? Nia yenu si nzuri. Kutumia mdomo mchafu, kudharau, kuita kafiri na dajali, kuapiza, kuongopa na kudhihirisha ushindi wa uongo, je kwa njia hii ushindi wowote unaweza kupatikana; bali sikuzote Manabii na wakweli waliendelea kusikia maneno kama hayo kutoka kwa

wenye shari. Ikiwa mnamtegemea Mungu kwamba Yu pamoja nanyi, basi chapisheni bishara yoyote kutoka Kwake, na kwa kukabiliana nayo tazameni kutoka kwetu; la sivyo kaeni kama mfu mkangoje wakati. Kama ni kutusi tu, siwezi kufumba mdomo wenu, wala Hadhrat Musa[as] aliweza kufumba midomo ya watoao matusi wala Hadhrat Isa[as] aliweza kufumba wala Seyidna na Maulana Hadhrat Muhammad Mteule[saw] aliweza kufumba. Lakini kama yupo mtu mwema yeyote kati yenu, yeye anapaswa kutafakari kwamba kwa kukubali madai yangu, jazba yenye harara yaendelea kuzuka ndani ya Waislamu kuanzia Peshawar mpaka Rawalpindi, Jhelum, Gujrat, Sialkot, Gujranwala, Wazirabad, Amritsar, Lahore, Jalandhar, Ludhiana, Ambala, Patiala, Delhi, Ilahabad [Prayagra], Bombay, Calcutta, Madras, Hyderabad Deccan; ilmuradi, nieleze mpaka wapi. Tazameni miji yote na vijiji vyote vya Panjab na India, kwa nadra tu utakuwa mji usio na mwanajumuiya. Sasa kama ipo huruma ya kweli kwa Waislamu, basi mambo haya maovu hayatoshi kwamba Mirza hakuweza kujibu, ameshindwa mara nyingi wala hakupata muradi wake. Sasa kwa wafahamivu uongo kama huo unanuka sana kuliko mzoga; na mtu mwema hataupenda. Mara nyingi Mabaniani, matopasi na watu duni sana wanasema mara nyingi kwamba tumewanyamazisha Waislamu katika mazungumzo ya dini, nao katika kila mkusanyiko wetu

walishindwa wala hawakupata muradi wao. Lakini mtu mwema anapaswa kuchukia uongo mchafu wa namna hii. Ee mpendwa, kama imo hata chembe ya huruma ya Waislamu moyoni mwako, basi sasa sio wakati wa upayukaji huu. Sasa kwa kweli yapasa kufanya mashindano ili mwongo adhalilike.

**Kauli yake**: Kwa kudhalikika katika mubahala, hastahili kushughulikiwa na kujibiwa na Maulamaa wakubwa na Masufii waheshimiwa.

**Nasema**: Ni masikitiko kwamba kwa kutaja mubahala na kusema uongo uchukizao umejidhalilisha zaidi na kujiaibisha. Siwezi kuelewa kwamba haya yenu imepotea wapi, na kwa nini mmekuwa adui wa takwa na kusema kweli. Tafakari kwamba kadiri wewe na Jumuiya yako ilivyoanza kurudi nyuma, hiyo imeanzia baada ya siku ya mubahala. Hii ilikuwa ni ishara kubwa ya ukweli wangu, ambayo kwayo hujajifaidisha hata kidogo kwa bahati yako mbaya. Sijui mmekaa ndani ya pango gani kwamba hamna habari kamwe za hali ya dunia. Maelfu ya watu wamepata kusema kwa sauti kuu na roho zisizohesabika zimeshahisi kwamba siku ya ushindi na maendeleo yetu na ya kurudi nyuma kwenu na kushuka chini, ilikuwa tu siku ya mubahala. Angalia mfano mdogo kwamba siku ya mubahala, bali wakati ule ule hadharani, ulipoisha mubahala na bado wewe na mimi tulikuwepo uwanjani humo humo na watu wote walikuwepo, Mwenyezi

Mungu kwa kudhihirisha heshima yangu mbele ya mkusanyiko wa watu Alikudhalilisha na kukufedhehesha papo hapo. Yaani, akamsimamisha mara shahidi mmoja kutoka katika jumuiya yako. Yeye alikuwa nani? Munshi Muhammad Ya'kuub nduguye Hafidh Muhammad Yusuf. Yeye akaapa, akilia akaniambia akisema, "Nashuhudia u mkweli, kwani nimeshasikia kutoka kwa Sheikh Abdallah Ghaznawii kwamba wakati wa kueleza tafsiri ya ndoto alikusadikisha na akasema, nuru moja imeshuka kutoka mbinguni, naye ndiye Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian. Sasa angalia, bado ulikuwa hujaondoka penye mubahala, Mungu akakudhalilisha. Na mtu ambaye unayo fahari ya kuwa ni mwalimu wako, yeye ndiye akashuhudia kwamba u mwongo na Ghulam Ahmad wa Qadian yu mkweli. Sasa zaidi ya hiyo, athari gani ya mara moja ya mubahala itakuwa kwamba Mungu Akadhihirisha heshima yangu wakati huo, na ulipatikana wakati ule ule ushahidi wa ukweli wangu na ushahidi wenyewe wa mwalimu wako, yaani wa Abdallah Ghaznawii ambaye ukikataa kauli yake utaitwa عَاق [yaani utatolewa katika urithi wake], kwani heshima yako yote inamtegemea yeye; ukimfahamu kuwa mwongo basi u mwanafunzi mwasi. Ilmuradi, hii ilikuwa ni ishara ya Mungu kwamba mara baada ya mubahala uwanjani mumo humo, wakati uo huo, saa iyo hiyo Mungu Akakudhalilisha na kufedhehesha na

kudhihirisha kushindwa kwako kwa ushahidi wa mwalimu wako kwa kupitia mtu wa jumuiya yako. Kisha baada ya mubahala ishara nyingine ya heshima yangu ikatokea ambayo malaki ya watu ni mashahidi wake, nayo ndiyo hii kwamba kwa Jumuiya yangu nilipata ushindi wa kifedha kiasi hiki kwamba kama ningetaka ningeweza kununua sehemu kubwa ya Ghazni, na daftari za Posta za serikali ni shahidi zinamoandikwa hawala za fedha. Lakini, je ulipokea hawala ya fedha ya hata *Anna* mbili baada yake? Kama imefika, basi lete uthibitisho wake. Sasa swali ni hili kwamba hizi rupia maelfu nilizoletewa baada ya mubahala zisizopungua rupia elfu thelathini, je sio uthibitisho wa jambo hili kwamba Waislamu waliniheshimu na wakinipenda walinitolea mali zao? Hii ni ishara adhimu ambayo kuipinga ni kujidhalilisha. Kisha ishara ya athari ya mubahala ni hii kwamba Jumuiya ya watu elfu thelathini iliyo pamoja nami imepatikana baada ya mubahala. Kufa kwa Atham na kuaga dunia kwa kuacha kuipinga Islam kwa kudumu ilitokea sawa na bishara baada ya mubahala tu. Lengo la bishara lilikuwa kwamba kati yetu wawili mwenye dini ya uongo atakufa kabla ya mwenzake. Basi, Atham kwa kufa kabla yangu akapiga muhuri juu ya ukweli wangu. Kisha, baada yake, ishara ya Lekhram kuuliwa ilidhihirika ambayo watu wapatao elfu tatu, Waislamu na Mabaniani, walishuhudia kwa

kutilia saini orodha ya mashahidi iliyotayarishwa nasi kwamba bishara hii imetimia dhahiri shahiri. Kwenye orodha hii kuna saini ya Seyid Fat'he Shah, Ofisa msaidizi wa mambo ya mifereji, akiwa katika jumuiya ya wapinzani akasadikisha. Ni jambo la yakini kwamba watu wapatao elfu thelathini kwa kushuhudia ukweli wa bishara hii wakaamini, waila Jumuiya yetu kabla ya mubahala haikuwa na idadi zaidi ya mia tatu. Kisha baada ya ishara za Mwenyezi Mungu zikanyesha kiasi hiki kwamba ishara zaidi ya mia zikadhihirika ambazo watu lukuki ni mashahidi wake. Matajiri na wafanyabiashara wakubwa wakubwa walijiunga na Jumuiya hii, na halaiki ya watu wakanikimbilia kwa kunipenda na kuniamini na kibali adhimu kikaenea ardhini. Je, humo haikuwa dhila yako? Mtu aliyekaa mbali ni kama kipofu; kama ukija Qadian kwa wiki moja au mbili kuona jinsi watu wanavyofika kutoka kila upande wakisafiri maelfu ya maili, na jinsi wanitoleavyo maelfu ya rupia, na jinsi kutoka kila nchi zawadi zenye thamani na vitu vya tunu na matunda yanavyofika, na jinsi nyumba ya wageni ilivyoandaliwa kwa ajili ya mamia ya watu, na jinsi katika msikiti wetu wa Ijumaa mamia ya watu waliojiunga na Jumuiya wanasali sala ya pamoja, na jinsi wajao kunizuru wasiohesabika huonyesha unyenyekevu, basi hali hiyo ukiona pengine itasababisha kifo chako cha ghafla kwa huzuni kubwa

sana. Sasa tafakari kwa uadilifu kwamba nani amefeheheka na kudhalilika na nani ameheshimika. Kama ungejua kwamba kabla ya mubahala Jumuiya yangu ilikuwa kiasi gani na kibali changu kadiri gani, na kisha baada ya mubahala kibali kilienea ardhini kiasi gani na kadiri waliyojiunga watu makundi kwa makundi na Jumuiya hii tukufu, basi nilikuwa na yakini kwamba ungekuwa umekufa tangu zamani kwa huzuni kali ukiugua kwa kifua kikuu cha mapafu au kile cha kiungo kingine. Nasema nikiapa kwa Mwenyezi Mungu Ambaye kiapo chake cha uongo ni kazi ya mlaaniwa, na kukadhibisha kiapo changu hiki pia ni kazi ya mlaaniwa, kwamba heshima na kibali changu kabla ya mubahala kilikuwa kama tone moja na sasa baada ya mubahala ni kama mto.

Ilmuradi, kwa kila jiha Mungu Akanisaidia kiasi hiki kwamba nikipokea ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu nilichapisha bishara moja katika vitabu vyangu kwamba Abdul Hak Ghaznawii hatakufa kabla hajazaliwa mwanangu wa nne. Basi, alhamdulillahi, yeye pia akazaliwa katika uhai wako ambaye jina lake ni Mubarak Ahmad. Na kadhalika karibu ishara zingine mia zilidhihirika na nikapata heshima juu ya heshima mpaka maadui wakiona heshima yangu kuwa adhabu kwao wakanishtaki pia mahakamani kwa kuchomwa na husuda, lakini katika kila uwanja walishindwa na

kudhalilika. Sasa, niambie umepata baada ya mubahala heshima na kibali gani, na kiasi gani watu walijiunga na kiasi gani ulipata ushindi wa mali, na ulipata watoto wangapi. Basi, mubahala wako ukamletea uharibifu Sheikh Abdul Wahid wa Jumuiya yako; nyumba yake pia ikaharibika kwa kifo cha mkewe. Mwenyezi Mungu Aliniahidi kwamba baada ya mubahala utajaliwa wana wawili wengine, basi wameshazaliwa wawili wengine na bishara zile mbili zikatimia walizosomewa mamia ya watu. Sasa, sema, bishara zako zimeenda wapi? Ebu, jibu kwamba baada ya upayukaji wako wana wangapi walizaliwa? Ebu, sema kwa uadilifu kwamba baada ya kudai na kueneza kwa tangazo kuhusu mwana ulipokosa kupata muradi wako wala hukufanikiwa kabisa, je hii ilikuwa dhila au heshima? Na hakuna shaka ndani yake kwamba baada ya mubahala, kibali nilichojaliwa, hicho chote kilisababisha dhila yako.

**Kauli Yake**: Je imedhihirika natija yoyote ya bishara kuhusu Atham, mkwe wa Mirza Ahmad Beg na mwana wako aliyeahidiwa?

**Nasmea**: Maelfu ya watu wenye busara wameshakubali kwamba Atham alikufa sawa na bishara, na kama yu mzima basi mleteni. Ukisema hakufa ndani ya muda uliowekwa, basi huu ndio ujinga wako kudhani hivyo, kwani bishara ilikuwa na sharti na kwa kuwa sharti lilipotimia, muda ulifutika. Isitoshe, nakuuliza, je

unamwamini Nabii Yunus kuwa nabii mkweli au la. Kwa nini bishara yake haikutimia, ilhali kulikuwa hamna sharti lolote humo. Basi ikiwa una haya na imani, kwa nini unapinga bishara zenye sharti. Soma kitabu cha Nabii Yona na Durri Manthur, jinsi gani Nabii Yona akataabika kwa kutotimia kwa bishara. Sasa umlaumu Yunus[as] zaidi kuliko mimi, kwani bishara yake ya mkataa isiyokuwa na sharti lolote haikutimia. Enyi majahili, mbona mwaishambulia Islam. Ukweli ndio huu kwamba katika bishara ya onyo, Mwenyezi Mungu huwa na hiari kuiahirisha kwa kutubu, kuomba msamaha na kurejea, hata kama isiwe na sharti lolote. Kama isiwe hivyo, kutoa sadaka, kutenda mambo ya heri na maombi yote yatabatilika, na kanuni hii iliyokubaliwa na Manabii wote kwamba يُرَدُّ الْقَضَاءُ بِالصَّدَقَاتِ وَالدُّعَاءِ , [Takdiri huondolewa kwa sadaka na dua] haitakuwa sahihi. Isitoshe, kila mwenye lubu aweza kutafakari kwamba ushindani kati yangu mimi na Deputy Atham haukuhusu madai yangu. Kiini cha majadiliano hayo yote kilikuwa ni hiki tu kwamba Atham alisema dini ya Kikristo ni kweli na – Mungu Apishe mbali – Nabii[saw] wetu ni mzushi, na Kurani si Neno la Mungu bali ni uzushi wa mtu. Nami nilisema kwamba dini ya Kikristo haikubaki katika hali yake ya mwanzo, na utatu na kafara na kadhalika yote ni batili. Basi, siku kumi na tano za majadiliano zilipoisha, siku ya mwisho, jinsi Mwenyezi Mungu Alivyonifunulia,

nikamwambia Atham ndani ya hafla ya mjadala huo walipokwepo Waislamu na Wakristo zaidi ya sabini, kwamba umemwita Nabii[saw] wetu dajali katika kitabu chako, na kwamba Islam ni dni ya uongo. Na angalia, wakati huu umejadiliana ukiwa mtetezi wa dini ya Kikristo, nami nikifahamu Islam kuwa ya kweli nimejadiliana kuitetea. Sasa kwa kupata ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu nasema kwamba kati yetu sisi wawili, anayeitetea dini ya uongo atatupwa katika *hawiya* katika uhai wa mkweli, yaani atakufa. Lakini aliye mtetezi wa dini ya kweli atabaki salama. Na mwongo atakufa katika miezi kumi na mitano asiporejea hata kidogo kwenye haki. Nilipoeleza bishara hii ambayo muhtasari wake ni huo, papo hapo Atham akatoa ulimi na akainua mikono miwili kama watubiao na kadhihrisha majuto yake kwa kuita dajali. Basi, bila shaka, kutoka kwa Mkristo, huku ni kurejea ambako Waislamu na Wakristo zaidi ya sabini ni mashahidi wake. Na baada yake, kwa miezi kumi na mitano kukaa kwa Abdallah Atham upwekeni, na kuacha kukaa na Wakristo wa Amritsar, na kutoshtaki licha ya kuwa na haki ya kushtak kisheria, na kukiri kwamba simwamini Hadhrat Masihi kuwa mwana wa Mung kama watu hao, na kukataa kuapa licha ya kuahidiwa zawadi ya rupia elfu nne, na kutoandika hata neno moja kupinga Islam katika muda uliowekwa kutimia bishara, na kudumu

kulia na kuacha kujadiliana na Waislamu kinyume cha mazoea yake ya zamani, mambo hayo yote ndiyo ambayo kama mtu si mkorofi na mwenye moyo mweusi, atakuwa hana budi kufahamu kwamba Abdallah Atham bila shaka akaogopa baada ya kusikiliza bishara na akawa na adhama ya Islam moyoni. Hivyo, ilikuwa lazima kufaidika na sharti la ufunuo sawa na kiasi cha kurejea kwake. Tena, kwa kutojali mambo hayo yote, ni Mwislamu wa aina gani yule mtu ambaye katika mjadala wa kidini wa aina hii ambamo kushindwa kwangu huiathari vibaya Islam, hata hivyo anaendelea kusema kwamba Wakristo walishinda na bishara ikathibitika kuwa uongo. Ee mjinga ikiwa bishara ikathibitika kuwa uongo, yakupasa uingie Ukristo, kwani katika hali hii dini ya Kikristo imethibitika kuwa ya kweli. Ilikuwa ni jambo la fahari sana kwenu kwamba watu wawili kutoka dini mbili walisimama kukabiliana na Islam, yaani Atham na Lekhram. Nao wakaambiwa uamuzi wa kimbingu kwamba mtu anayefuata dini ya uongo atakufa kabla ya yule anayefuata dini ya kweli. Basi, katika uhai wangu Atham na Lekhram wtoe wawili walikufa, na mimi kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu mpaka sasa ni mzima. Na kama Islam isingekuwa kweli ingewezekana, bali lazima ningekufa kabla yao. Basi, Mwogopeni Mungu, na ushindi ule iliopata Islam kwa fadhili kubwa ya Mungu msiueleze kama ushinde kwa

kunihasidi. Tazameni, Atham yuko wapi sasa na Lekhram yupo katika nchi gani. Je si kweli kwamba miaka kadhaa imepita alipofariki Atham na kaburi lake lipo katika Ferozpur. Basi lengo hasa la bishara, yaani kufa kwa Athma katika uahi wangu, limeishatimia, kwa nini mnalia mkitaja muda mara kwa mara na kusema kwamba kweli amekufa lakini hakufa ndani ya muda uliowekwa. Huu ni udhuru mbovu wa aina gani. Enyi wajinga na msioelewa siri za sheria ya Mungu, ambapo katika bishara ya onyo Mungu anayo hiari hii pia kwamba kwa toba na kurejea Huondoa adhabu kabisa, basi je kupunguza kidogo muda au kuongeza kwaweza kuzusha ukinzani? سُبۡحٰنَ اللّٰہِ عَمَّا یَصِفُوۡنَ[12]. Na ni dhahiri kwamba Mwenyezi Mungu Hataki kuficha rehema yake na kupendelea kufanya ukarimu. Basi, Atham aliposikia tu bishara papo kwa papo akainamisha kichwa na akitoa ulimi na kuinua mikono miwili akadhihirisha athari za toba na majuto ambayo shahidi wake ndiye daktari Martin Clarke pia, na walikuwepo waheshimiwa wengi Waislamu na Wakristo akiwemo, sawa na kumbukumbu yangu, Khan Muhammad Yusuf Khan, Chifu wa Amritsar pia miongoni mwa waliokuwepo wakati ule, basi je kurejea huko hakukutimiza sehemu yoyote ya

[12] Mwenyezi Mungu ni Mtakatifu, Ameepukana na sifa wanazomsifu. Al-Mu'minuun 23:92

sharti? Nasema kweli kabisa kwamba ukinzani ungezuka kama licha ya Athma kujinyenyekeza na kuogopa na kujidhalilisha na licha ya kuwa kama mwenye wazimu kwa huzuni na kufumba mdomo wake, Mwenyezi Mungu asingempa nafuu ya sharti lake hata kidogo na kwa ukali sana Angemfisha ndani ya muda uliowekwa. Je hayapatikani maarifa ya sifa tukufu za Mungu kwamba Akamfaidisha Atham kwa sababu ya unyenyekevu na hofu yake pia na kisha sawa na lengo la bishara Akakatisha roho yake ili ithibitike kwamba kiasi alichodhihirisha unyenyekevu na hofu, malipo yake kidhahiri yangekuwa kupewa maisha kwa akali miaka kumi ili angepata malipo kamili ya hofu ya moyoni mwake sawa na aya مَنْ يَّعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَّرَهٗ[13]; lakini, Mwenyezi Mungu Akamfisha haraka ili mapadri wasipate kuwadanganya watu wasioelewa wala wasiufanye uhai wake kuwa ushahidi wa ukweli wa dini yao. Nilihofia wakati ule Atham alipotoa ulimi wake katika mkusanyiko wa hadhara na akiwa na huzuni akiinua mikono yake miwili na kudhihirisha anamheshimu Mtume Mtukufu[saw]. Na nikafikiri wakati ule ule kwamba sasa mtu huyu kwa kujuta ameanguka kizingitini pa Mungu Rahimu, tuone natija yake itakuwa

[13] Basi anayefanya wema sawa na chembe, atauona. Az-Zilzaal 99:8

nini. Kwani, nalijua Mungu Yu Rahimu na kwa sababu ya sifa yake hiyo Nabii Yunus akapata jaribio, na wale aliowaahidi adhabu ya kuhilikisha katika siku arobaini hawakudhurika hata kidogo. Na ikumbukwe kwamba watafutao haki wanapata faida ya kielimu pia kutoka katika bishara hii na bishara kuhusu Lekhram. Na ile faida ya kielimu ndiyo hii kwamba bishara kuhusu Atham kwa sababu ya kuogopa kwake na kuhofia ikadhihirika kwa sura ya *Kijamali*, na bishara iliyokuwa kuhusu Lekhram, hiyo kwa sababu ya utovu wa adabu, ujeri na mdomo mchafu uliozidi baada ya bishara, ikadhihirika kwa sura ya *Kijalali*, na 'kisu' cha ulimi wake hatimaye kilimmaliza.

Hayo tumeeleza kuhusu Atham; na kumhusu mkwe wa Ahmad Beg tumeshaeleza mara kwa mara kwamba bishara hii ilikuwa na sehemu mbili; moja kuhusu kifo cha Ahmad Beg, na nyingine kumhusu mkwe wake. Basi, mmeshasikia kwamba muda mrefu umepita Ahmad Beg alipofariki sawa na bishara, na kaburi lake lipo huko Hoshiarpur. Na mkwe wake, kwa sababu ya sharti la bishara mauti yake yakaahirishwa, na tumeshaeleza kwamba bishara ilikuwa na sharti. Basi, Ahmad Beg, kwa kutojali sharti alipofariki, mauti yake yakawapa nafasi mkwewe na jamaa wengine kwamba waogope na wanufaike na sharti. Na ikawa hivyo hivyo. Na ufunuo kuhusu Ahmad Beg na mkwewe ibara yake

ilikuwa hii اَيَّتُهَا الۡمَرۡأَةُ تُوۡبِیۡ تُوۡبِیۡ فَاِنَّ الۡبَلَاۤءَ عَلٰی عَقِبِكِ. Nakumbuka kwamba ufunuo huu, hapo kabla, alisomewa mtu mmoja wa Jumuiya yako aliyeitwa Abur Rahim au Abdul Wahid huko Hoshiarpur nyumbani mwa Sheikh Mehr Ali, alipokwepo Hafidh Muhammad Yusufu au Munshi Muhammad Ya'kub na Munshi Ilahi Bakhsh, na baadaye ufunuo huu ulichapishwa pia. Ilimuradi, bishara hii ilikuwa na sharti kama vile bishara kuhusu Atham ilikuwa yenye sharti. Na hata kama isingekuwa na sharti, hata hivyo kwa sababu ya kuwa ya onyo, ingefanana na bishara ya Nabii Yunus. Na yapasa kuona matokeo ya maneno ya Mungu kwa subira sio kwa kupinga kwa nia ya shari.

Na swali kuhusu mwana aliyeahidiwa, linathibitisha hii tu kwamba akili ya wapinzani wetu imepotea hata kwamba wakati wa kupinga hawakumbuki kwamba upo wakati wa kufaa wa kupinga au hapana. Ewe mjinga, kama Mwenyezi Mungu Alivyoahidi, Akamjalia wavulana wanne, na kabla ya kuzaliwa kwa kila mwana Akanipasha kwa ufunuo wake maalumu habari ya kuzaliwa kwake, na bishara hizo zote nne zilichapishwa na kuenezwa duniani kabla ya wakati, ambazo malaki ya watu katika nchi hizi ni mashahidi wake. Basi, siwezi kuelewa ukinzani wenyewe ni nini? Ukinzani unazuka juu ya hali yako kwamba ulitamka mdomoni ya kuwa kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu utapata mwana na

ukachapisha bishara hii katika tangazo, kisha mvulana yule akayeyuka ndani kwa ndani, wala hakuweza kutoka nje; laiti angezaliwa hata akiwa mfu ili ungekuwa na la kusema. Hii pia ni athari mbaya ya mubahala uliyopata kwamba umekosa kizazi. Ilmuradi, kwangu wavulana wanne walizaliwa baada ya bishara; na kabla ya kuzaliwa kila mwana, Mungu Alipasha habari niliyotangaza baina ya maelfu ya watu; lakini sema wewe, nani alizaliwa katika nyumba yako? Bado upo chini ya lawama. Laiti usingefanya mubahala na mkweli, hapo labda kwa sasa ungekuwa umeishapata mwana. Basi ona aibu yako katika kioo, hakuna nafasi ya kunipinga. Naam, ikiwa nilitangaza ufunuo wowote umaanishao kwamba kutokana na himila iliyo karibu na ufunuo huo na katika mwaka huo, mwana yule atazaliwa, basi utangaze ufunuo wangu huo. Lakini, jitahadhari, usilete upinzani kama ule ulioletwa na baadhi ya wanafiki kuhusu tukio la Hudaibia ambao kwao Mungu Alimlinda Umar Faruk na wanafiki waliangamia. Ewe mpendwa, mbona unaachana na sheria ya Muhammad[saw] kwa kunichukia mimi. Hapa huna pa kushikilia. Na licha ya itikadi hii iliyokubaliwa na wote kwamba pengine Nabii pia anaweza kukosea kuelewa wakati na mahali pa kutimia bishara yake, na kuhusiana na hiyo, maulamaa wanatoa ushahidi wa Hadithi ذَهَبَ وَهْلِيْ[14] , iliyopo katika Bukhari,

[14] Hadithi hii inaeleza kuwa Mtume[saw] aliona ndani ya ruya

wanaona kwamba kwa kosa la kutafsiri, bishara haiwezi kuwa uongo wala haiwezi kusemwa siyo iliyofunuliwa. Basi, kama bishara ya Manabii inao wasaa kiasi hiki kwamba tafsiri isiyo sahihi ya Nabii haiidhuru chochote bishara, basi ukinzani utakuwa hapo tu ambapo ufunuo uthibitishwe kubatilika kutokana na maneno ya ufunuo huo.

**Kauli yake**: Mirza anajua kwa yakini kwamba kwa kazi hii isiyofaa hatakuja yeyote wala kazi hii haitafanyika, mimi nitapata umashuhuri wa bure tu.

**Nasema**: Ewe usiyefahamu, Mwogope Mungu. Je, kazi ya dini unaiita kazi isiyofaa. Je Manabii wa Mungu waliendelea kushughulikia kazi isiyo na maana? Ee azizi, je hii ni kazi mbovu ambayo kwayo maelfu ya watu huokoka katika uongo na upotevu na mafarakano ya ndani ya umati huu yaliyodhoofisha Waislamu huondolewa. Ikiwa hii ni kazi bure, basi je kazi zingine zilikuwa za lazima kwa sheria mnazozifanya. Mathalan, Nadhiir Husain wa Delhi, juu ya kuwa mzee, alikuja Batala kwa harusi ya mwanaye Sheikh Muhammad Husain wa Batala na akaenda mpaka wilaya ya Sialkot. Alikuwa na lengo gani isipokuwa kula chakula. Katika zama hizi, hali ya Waislamu imedhoofika kwa sababu

---

kwamba anahamia penye mitende. Akasema nilifikiri ni Yamamah au Hajar, kumbe, ilikuwa ni Madina. Mwenezi

masheikh wa zama hizi wanazifikiria kazi za lazima kuwa kazi ya kipuuzi, na kwa shughuli za nafsi zao hutembelea mpaka Aden na Maskat, na hakuna anayeziona kazi hizo za bure. Lakini kazi za kusaidia Islam wanaziona si za lazima, bali kwa ajili ya kula nyama na pilau na kwa kushiriki katika karamu za arusi husafiri mamia ya maili. 'Mzuri' ulioje udini huu kwamba kwa upande mmoja wanapiga kelele kuwa watu elfu thelathini wanaendelea kuwa makafiri kwa kujiunga na Jumuiya hii, na wanapoambiwa njooni tukaamue twajibiwa kuwa maulamaa hawanayo fursa wala matumizi ya nauli kwa kazi hii bure. Wakati huu kwa kuwatimizia maulamaa kama hao hoja ya Mungu tupo tayari kuwasaidia nauli sawa na masharti yaliyoandikwa hapo juu. Laiti kwa njia yoyote mioyo yao inyooke. Islam hushinda dini zote. Hao wanayo Islam ya aina gani isiyoweza kuwapa utuvu. Ilmuradi, sasa tumeshavunja udhuru wao huu pia.

**Kauli yake**: Enyi Wakristo wapya na waanziliziwa kanisa jipya, twawaambieni njia nyepesi na rahisi sana.

**Nasema**: Ee mpita mipaka, je unawaita Wakristo wale Waislamu wanaoitetea Islam na ndio hoja ya Mwenyezi Mungu ardhini. Kama Waislamu wangekuwa kama wewe, basi Islam ingekuwa imefutika. Kisha baada yake umemtaja Maulawii Abdul Karim kwa masihara na dhihaka, na umeomba ishara hii kwamba bwana

Maulawii aliyetajwa aondokewe na udhaifu alionao katika mguu na tofauti ndani ya jicho moja. Na kwa kutaja huku, lengo lako hasa ni masihara na istihizai tu, na kauli hii ni kama ya makafiri ambao, Mungu Apishe mbali, walimwita Mtume Mtukufu[saw] mkiwa na kuomba ishara hii kwamba ikiwa yu Nabii mkweli, basi wanawe waliokufa awahuishe. Lakini tumeshajibu hivi punde mzaha huu. Ni dhahiri kwamba mtu kwa sababu ya ubinadamu wake anakuwa na kasoro hii au ile, na daima anashikwa na maradhi na shida, jamaa wanafariki pia; lakini hakuna mwungwana yeyote anayeudhi hivyo kwa kujisingiza kuomba ishara. Hii ni desturi ya watu dhalili na masafihi; na katika nchi yetu masihara ya aina hii wafanya *marasi*.[15] Hatujui kwa nini Mian Abdul Hak akafuata njia hii. Kama mtu akimlaumu Mian Abdallah Ghaznawii kwa mambo machache ya namna hii kwamba ikiwa yeye alikuwa mpokeaji ufunuo basi angepaswa aondoe baadhi ya kasoro zake yeye mwenyewe na kuonyesha watu ishara hii, hapo sijui kina Ghaznawii hao watajibuje. Ee azizi, ikiwa utawapa wengine udhia hiyo, basi huo utamfikia babako na mwongozi wako. Basi mambo haya ya kufitinisha

---

[15] *Marasi* au *Mirathi* ni mtu asiye na heshima anayewachekesha watu katika hafla za arusi na kadhalika kwa kufanya masihara na pia kuimba, na watu wanamtolea hela kuwachekesha. Mwenezi

yamefaa nini, bali mbele ya Mwenyezi Mungu wewe utakuwa mwenyewe kumdhalilisha babako na mwongozi wako. Na kama kwa kudra ya Mungu macho yako yote mawili yapatwe na maradhi ya mtoto wa jicho au miguu yako ipate kupooza, hapo utatambua masihara hayo yote. Enyi mlioghafilika, mbona mnawaaibisha wengine; je haiyumkini kwamba wakati fulani nyinyi wenyewe mpatwe na kasoro kama hizo za kimwili na watu wawaachekeni au kujitahadhari kuwaguseni. Mwogopeni Mungu wala msifuate nyayo za makafiri. Kumbukeni kwamba Manabii wote wamewaita maluuni wanaomba ishara wanazotaka kutoka kwa manabii na mitume. Angalia, Hadhrat Isa[as] aliyosema kwamba kizazi kibaya na cha zinaa cha zama hizi chataka ishara; hao hawataonyeshwa ishara yoyote. Kadhalika Kurani Tukufu imewaita maluuni waliokuwa wakiomba ishara walizopendekeza kutoka kwa Hadhrat Seyidna Muhammad Mteule[saw] waliotajwa mara kwa mara katika Kurani Tukufu wakilaaniwa, jinsi walivyosema فَلْيَأْتِنَا بِاٰيَةٍ كَمَآ أُرْسِلَ الْاَوَّلُوْنَ[16] , yaani tuonyeshwe ishara zile za Hadhrat Musa[as] au za Hadhrat Masihi[as], na pengine wakaomba ishara ya kupaa mbinguni, na pengine nyumba yako igeuke kuwa ya dhahabu; na daima wakakataliwa. Someni Kurani Tukufu tangu mwanzo mpaka mwisho,

---

[16] Al-Anbiyaa 21:6

hamtakuta hata alama ya jambo hili kwamba kafiri yeyote alitaka kutoka kwake kwamba rekebisha mguu au ponya jicho au huisha mfu, na Mtume Mtukufu[saw] akafanya hivyo. Pia haukupatikana mfano wake wowote katika Injili kwamba makafiri wakaja kuomba ishara nao wakaonyeshwa. Bali, safari moja Masahaba walimwomba Mtume[saw] kwamba mtu fulani aliyeoa juzi juzi amekufa kwa kuumwa na nyoka, umhuishe, hapo yeye akasema, nendeni mkamzike ndugu yenu. Ilmuradi, Kurani Tukufu imejaa jambo hili kwamba makafiri wachafu na waovu wa Makka walikuwa wakimwomba Mtume[saw] ishara za aina aina, na daima wakashindwa kukubaliwa swali hilo na kulaaniwa na Mwenyezi Mungu. Kadhalika soma Injili nzima kwamba waombao ishara sawa na matakwa yao wakalaumiwa na Hadhrat Isa[as]. Basi ewe azizi, Mwogope Mungu, umri hautegemewi. Mwenyezi Mungu Hudhihirisha ishara kwa mkono wangu, lakini sawa na suna ile Aliyowawekea Mitume wake tangu kale, bila shaka kwa kuzingatia suna hiyo mtu akija hata akiwa kama shetani, hata hivyo ataaminishwa kwa ishara za Mungu. Lakini, kama akitaka kinyume cha suna ya kale cha Mungu, basi hana hadhi yoyote katika neema ile na kwa yakini atakufa akinyimwa jinsi Abu Jahli alivyokufa akinyimwa. Ee azizi, unayo hiari kwamba kwa njia ile Aliyonituma Mwenyezi Mungu ulete kundi la vilema, walemavu, vipofu na wagonjwa wengine,

kisha kwa njia ya kura kundi Atakalonipatia Mungu, basi nikishindwa, nitastahiki matusi yale yote uliyotoa katika tangazo lako, waila matusi yale yote yatakurejea. Angalia, kwa njia hii pia utapata lengo lako. Basi, ikiwa huna nia ya ufisadi moyoni, kwa nini unafuata njia waliyoifuata wale walioitwa kizazi cha zinaa kwa ulimi wa Hadhrat Isa[as], na wenye Motoni na maluuni kwa ulimi wa Mtume Mtukufu[saw] kama unayo imani moyoni hata sawa na chembe, basi njia hii ninayotoa kutoka kwa Mwenyezi Mungu ina shida gani? Je utashinda kwa kutukana na kuita mkanamungu? Kwa yakini kundi lile litashinda la wale wasio wakanamungu na wanayo imani ya kweli juu ya Mwenyezi Mungu na wanajiepusha na mzaha na istihizai na hawaombi ishara sawa na matakwa yao kama makafiri wa zamani; bali wanatafakari juu ya ishara zilizoonyeshwa na Mwenyezi Mungu. Ee uliyeghafilikia mauti, mbona unakimbia njia ya uaminifu na unyofu, na kwa nini unatamka mambo ambayo kuhusu hayo hata moyo wako unakulaumu kwamba unasema uongo. Sema kweli, je bado hujajua kwamba ukimlazimisha Mungu kwa kumwomba jambo fulani kama kumtahini siyo njia ya watu wema; bali katika Neno la Mungu njia hii imeitwa uasi na utovu wa adabu. Soma Kurani kwa makini, kisha tafakari kwamba walioomba ishara sawa na matakwa yao wakajibiwa nini katika Kurani, na je walikuwa chini ya ghadhabu ya

Mwenyezi Mungu au chini ya rehema. Na ikiwa unayo haya kidogo na shauku ya kuchunguza haki, na kama u mkweli katika madai yako, basi upate fatwa kutoka kwa maulamaa wako wanaoelewa kidogo dini kwamba je Mungu Analazimika kwamba wakati kundi lolote la makafiri na wasiokuwa na imani wamwombapo Nabii au Muhadathi au Mtume awaonyeshe ishara ya kubuniwa nao, na kama asionyeshe basi Nabii yule aliyeombwa ishara kama hiyo atakuwa mwongo. Basi, ukipata fatwa hii kutoka kwa maulamaa, naahidi nitakuonyesha ishara uliyotaja. Na kama ukikosa kupata fatwa hiyo, basi adhabu hii ya uongo wako yatosha kwamba maulamaa wakubwa wa kaumu yako wamekukadhibisha. Na kwa upande wetu ukumbuke utabiri huu kwamba maulamaa mashuhuri kama Nadhiir Husain wa Delhi na Rashid Ahmad Gangohi kamwe hawatakupa fatwa hii hata kwa kulia mbele yao ujifie. Na wasomaji wanapaswa wasimwache mtu huyu anayebadilisha na kugeuza sheria ya Mungu mpaka alete fatwa kama hiyo ya maulamaa. Kwani, njia aliyoifuata kuomba ishara ndiyo kumfanyia Mungu mzaha na istihizai. Kumbukeni kwamba shetani ndiye wa kwanza kabisa duniani aliyetaka ishara kutoka kwa Hadhrat Isa[as] katika Baitul Mukaddas na akasema ujiangushe chini kutoka jengo hili; ukisalimika nitakuamini, lakini Hadhtar Masihi[as] akajibu, ondoka ewe shetani, kwani

imeishaandikwa kwamba usimjaribu Mungu. Hapo padre mmoja ameandika katika maelezo ya Injili kwamba kwa hakika huyo alikuwa ni mtu aliyetaka ishara sawa na matakwa yake kutoka kwa Hadhrat Masihi[as], na Hadhrat Masihi[as] mwenyewe akamwita shetani, kwani akataka kumtiisha Mungu kwa matakwa yake. Basi, sawa na kisa hiki cha Injili ni pa kuhofia sana kwa Mian Abdul Hak. Mtu asiponena kwa uaminifu, anatiishwa na shetani, kana kwamba anakuwa mwenyewe shetani, na aya hii ndiyo inayoishuhudia: مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ[17].

**Kauli yake**: Mirza na Wamirizai hawaamini Kiama, siku ya malipo, Pepo na Jahanamu, bali wanaonekana kuwa wakanamungu. Kwani, anayeamini Kiama hawi mdanganyifu, mwenye kumzulia Mungu, Mtume[saw] na watu uongo.

**Nasema**: Nasema kweli kabisa kwamba sifa hizo zote zimo ndani yenu, bali m wabaya zaidi kuliko wamkanao Mungu, kwani mkanamungu katika mawzo yake batili hapati ushahidi juu ya uwepo wa Mwenyezi Mungu; lakini nyinyi mkiishadai imani kisha mmnasema uongo wa kuchukiza, kwani mnaposema kwamba Hadhrat Isa[as] amekwenda mbinguni akiwa hai kwa mwili wake, hapo mnamzulia uongo waziwazi Mungu na Mtume[saw] wake.

[17] An-Naas 114:7

Na ikiwa hamuwazushii uongo, basi semeni kwa kiapo cha Mungu kwamba imeandikwa wapi katika Kurani Tukufu kwamba Hadhrat Isa[as] hajafa. Ni masikitiko kwamba unasoma katika Kurani Tukufu aya فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِىْ[18] na unajua vizuri kwamba katika Kurani Tukufu nzima kila sehemu neno ***Tawafii*** lamaanisha kutakabidhi roho. Na kadhalika unayo yakini kwamba katika Hadithi zote pia ***Tawafii*** lina maana ya kutakabidhi roho, kisha unasema kwa uzushi kwamba sehemu hii ***Tawafii*** lamaanisha kunyanyua mzima mzima. Kwa hiyo, ikiwa humzulii Mtume[saw] uwongo, basi sema na lete Hadithi isemayo kwamba Hadhrat Isa[as] alikwenda mbinguni mzima-mzima kwa mwili wake. Hae masikitiko, uongo na uzushi kiasi hiki! Enyi watu, je hamtakufa? Je hamtaingia kaburini abadan?

از افتراء و کذب شماخوں شد تست دل ہیچم     داند خدا کہ زیں غم دیں چوں شدست دل
ہیچم عیاں نشد کہ شما را بکینہ ام     زینساں چرا دلیر و دگرگوں شدت دل

[Tafsiri: Kwa uzushi na uongo wako moyo umehuzunika sana; Mungu ndiye Ajuaye sana hali ya moyo wangu ikoje kwa huzuni hii.

Sikuweza kujua kwamba kwa sababu ya uadui wangu, kwa nini moyo wako umejasiri dhidi yangu kiasi hiki.]

---

[18] Al-Maaida 5:118

Kisha, isipothibitika kwa Hadithi kwamba Hadhrat Isa[as] alikwenda mbinguni kwa mwili wa udongo au atashuka kutoka kwa mbinguni kwa mwili wa udongo; na Kurani Tukufu inamwingiza katika watu walio chini ya *Tawaffi*; na Hadithi ya *Mi'raji* inaunga mkono jambo hili, kwani usiku wa *Mi'raji* Mtume Mtukufu[saw] alimwona Hadhrat Isa[as] katika roho za waliokufa; na umri wa miaka 125 ulioelezwa katika Hadithi unafafanua waziwazi kwamba Hadhrat Isa[as] baada ya kupita muda huo lazima akafariki; vile vile katika Hadithi ya *Kanzul-Ummaal*, ambayo kwayo inathibitika kwamba baada ya tukio la msalaba Hadhrat Isa[as] alihamia nchi nyingine, inaiunga mkono; basi huu ni uzushi kiasi gani juu ya Mungu na Mtume[saw] kwamba mpaka sasa hamjizuii kuamini uongo huu! Kama Masihi yule yule angepaswa kurudi tena duniani, Mwenyezi Mungu Asingemwita mfu; na sehemu yoyote ya Hadithi ingeelezwa kwamba Hadhrat Isa[as] amekwenda mbinguni akiwa hai kwa mwili wake na wakati fulani atashuka akiwa hai pamoja na kiwiliwili chake. Lakini, sasa Hadithi zote zimeisha angaliwa; haijulikani wakati fulani Hadhrat Isa[as] akapaa mbinguni mzima pamoja na mwili na kisha atashuka kutoka mbinguni mzima na kiwiliwili chake. Na katika sifa ya atakayeshuka imeandikwa kuwa إِمَامُكُمْ مِنْكُمْ [Imamu wenu kutoka miongoni mwenu], lakini haikuandikwa kwamba إِمَامُكُمْ مِنْ أَنْبِيَاءِ بَنِيْ إِسْرَائِيْلَ [Imamu wenu kutoka miongoni mwa

Manabii wa wana wa Israeli]. Sasa tafakari kwamba Kurani na Hadithi zote mbili zinamlaani nani kwa sababu ya uzushi; sisi au nyinyi? Ikiwa unalo jibu la kupinga uthibitisho wetu huu, basi lete; la sivyo bila shaka u mzushi mbele ya Mungu. Na tena jambo haliishii hapo tu, bali katika mambo yote uzushi wako ni dhahiri, na ndimi zenu zi chafu kwa kusema uongo. Ebu, sema kuhusiana na mubahala ulinifanyia nini; kiasi gani ulisema uongo mara kwa mara na ukasema ukashinda katika mubahala. Ewe adui wa ukweli na aliyejitenga na haya, tafakari na tambua kwamba Mwenyezi Mungu Alikudhalilisha papo hapo kwa ushahidi wa Munshi Muhammad Yakub. Je, huu ulikuwa ushindi wako kwamba mwalimu wako Abdallah Ghaznawii alitoa ushahidi wa ukweli wangu? Sasa, kama mimi ni mzushi na sina imani juu ya Kiama, siku ya malipo na Jahanamu, basi papo hapo utalazimika kuamini kwamba mwalimu wako abdallah Ghazanawii alikuwa mzushi zaidi kuliko mimi, wala hakuwa na imani juu ya Kiama, siku ya malipo, Jahanamu na Pepo, kwani sawa na usemi wako, yeye alimwita mtu aliyemzulia Mungu uongo kuwa mkweli na kutoka kwa Mungu. Ewe mjinga, matusi yako haya yote yanakurejea usipothibitisha kwamba ushahidi aliotoa mwalimu wako Abdallah si sahihi. Ee mdhalimu, kwa nini unamwasi mwalimu wako. Ilikupasa kunikubali kabla ya wote,

kwani hata katika tangazo hili pia umeandika pamoja na jina lako maneno haya: "Abdul Hak Ghaznawii, mwanafunzi wa Hadhrat Maulana Maulawii Abdallah Ghaznawii." Ewe mtovu wa adabu, je ilikupasa kumpatia mwalimu wako malipo haya kwamba yule anayemwita mkweli ukamwita kadhabu? Na kwa kuwa sawa na upinzani wako huu Abdallah Ghaznawii amekuwa mzushi, na pasipo haki kwa kuongopa aliniita dhihirisho la nuru za Mungu, basi sasa unapaswa kujifia kwa haya, kwani u mwanafunzi wa huyo mzushi. Sisemi kwamba Maulawii Abdallah Ghaznawii alikuwa mzushi wala simwiti kadhabu na mdanganyifu, lakini bila shaka umemfanya mzushi. Mungu Akupe upatilizo wake kwamba ulimwita mtu mwema kama huyo kuwa mwovu. Kwani, anaponifahamu kuwa mkweli na kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na kwa kauli yako mimi ni mzushi, kadhabu na dajali, basi majina hayo yakamfikia Abdallah pia kama 'zawadi' kutoka kwako. Lakini, mtu akusikitikieje, kwani licha ya Abdallah hata ukamwita mwongozi wake pia kuwa mzushi. Kwani, Bwana Mian wa Kotha aliyekuwa mwongozi wa Maulawii Abdallah, akausia karibu na kifo chake kwamba Mahdi anakaribia kudhihiri katika Panjab, bali ameshazaliwa na sasa tupo katika zama zake.[19] Watu waliosomewa kashfi hii bado

[19] Ingawa Bwana Mian alipata kutamka neno Mahdi tu kwamba ameshazaliwa na lugha yake ni Kipanjabi, lakini wasikilizaji, sawa

wapo wazima mpaka sasa. Lakini, usiyetambua haki, hukujali adabu ya mwongozi wa mwongozi. Basi, 'heko', ulimfanyia 'wema' sana mwongozi wako na mwongozi wa mwongozi wako, na ukawaita wazushi na kadhabu. Kama wazao wa Maulawii Abdallah wanamheshimu baba yao, basi yapasa wamwondoe mara moja mtu kama huyo katika Jumuiya yao, kwani ampingaye mwalimu na mwongozi wake, hana heri ndani yake. Ewe mtovu wa adabu, je unamkosea adabu mzee ambaye unakiri kuwa mwanafunzi wake. Na kama ukijibu kwamba Munshi Muhammad Yakub ni shahidi mmoja tu, basi usikilize bishara hii pia ya pili. Kwa kuwa ilikuwa hakuna budi kwamba baada ya mubahala, Mungu Akudhalilishe kwa njia zote na Adhihirishe fedheha yako duniani, kwa hiyo siku hiyo hiyo tulipomaliza mabahala, au labda keshoye jioni, Hafidh Muhammad Yusuf, Inspekta wa Mito, mnayemwamini nanyi nyote kuwa mwema, akanilaki na mbele ya kundi kubwa la watu wapatao mia, akashuhudia kwamba Maulawii Abdallah alinielezea kashfi yake moja kwamba: Nuru moja imeanguka kutoka mbinguni na imeshukia Qadian, na kizazi changu kikanyimiwa hiyo, yaani watu

---

na karina, walielewa kwamba amemaanisha Mahdi Mau'udi, kwani wakatu huo huyo tu alingojewa; na usemi wa watu ni kwamba mtu anaposema, Mahdi atadhihiri lini, basi anamaanisha Mahdi Mau'udi na hivyo tu msikilizaji anaelewa. Mwandishi.

hao hawatamkubali na watakuwa wapinzani na watakosa kupata baraka hii.[20] Hafidh Muhammad Yusuf bado yu mzima. Uitishe kikao na nialike huko, kisha uwaulize kwa kiapo cha Mungu wazee hao wawili kwamba je matukio hayo mawili wameyaeleza au hapana; na hao wawili wanatokana na Jumuiya yako, nao pia ni walezi na wahisani wa Maulawii Abdallah. Sasa sema namna ilivyobanwa sana roho yako na kuthibitika waziwazi kwamba wewe ndiwe mzushi. Mungu Awalinde mahuluku yake na mamo yako ya uzushi. Amin.

---

[20] Inaonekana, kashfi hii ni ya zama nilipoonana na Maulawii Abdallah kule Khairawii katika zama za awali za umri wangu na nikaiona kuwa nimepata heri na wema. Hapo nikamwomba Bwana Abdallah kuniombea. Basi yeye katika joto kali wakati wa mchana akaenda nyumbani na kuniombea, na akanisomea ufunuo wake mmoja, nao ni huu kwamba اَنۡتَ مَوۡلَانَا فَانۡصُرۡنَا عَلَى الۡقَوۡمِ الۡكَافِرِيۡنَ . Na wakati wa adhuhuri baada ya kurudi kutoka nyumbani, akitabasamu akaniambia kwamba ilikuwa si kawaida ya Mungu kwangu iliyodhihirika kuhusiana na habari yako, na akasema katika lugha yake ya Kiajemi kwamba kwa ufunuo huu inafhamika kwamba kwa namna ya Masahaba, utaendelea kuwa na msaada wa Mungu. Kisha, nilipofika Qadian, akatuma barua kupitia posta alimorudia ufunuo huo, na labda baadhi ya sentensi nyingine pia. Basi, inaonekana Bwana Maulawii huyo kwa tukio hilo na mwelekeo huo akaona nuru ikishuka juu ya Qadian. Alikuwa mja mwema. Mungu Amrehemu. Amin. Mwandishi

**Kauli yake**: Vitabu vya Mirza vimejaa uongo na uzushi, na amwaminiye Mungu hawezi kujasiri hivyo.

**Nasema**: Kauli hiyo kwa maneno mengine yamaanisha kwamba Abdallah Ghaznawii akimwita mzushi kuwa mkweli na kutoka kwa Mungu, amesema uongo na uzushi hata kwamba amwaminiye Allah hawezi kujasiri hivyo. Sasa sema kweli, Ee Mian Abdul Hak, je mwaminio wa Mungu anaweza kujasiri hivi alivyofanya Mian Abdallah kwamba akamwita mzushi kuwa mkweli na nuru ya mbinguni. Mwenyezi Mungu Huwalaani wazushi. Basi, yule aliyezua ufunuo na kashfi ya uongo ya namna hii kwamba nuru ya Mwenyezi Mungu ilimteremkia Mirza Ghulam Ahmad Qadiani na kizazi changu wamenyimwa hiyo, kumhusu mtu huyo mwatoa fatwa gani? Lazima fatwa hii itangazwe. وَ مَنْ اَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرٰی عَلَی اللّٰہِ کَذِبًا[21]. Ulipiga kelele kwamba – Mungu Apishe mbali – nimesema uongo. Sasa imethibitika kwa ikirari yako kwamba Abdallah Ghaznawii mara nyingi akisema uongo juu ya Mwenyezi Mungu na kumzulia uwongo akaondoka dunia hii: na nani anaweza kuwa mbaya zaidi kuliko yule anayemzulia Mungu uongo.

[Ubeti wa Kiajemi]:

مرا خواندی و خود بدام آمدی      نظر پختہ تر کن کہ خام آمدی

[21] Al-An'aam 6:94

[Tafsiri: Uliniita, lakini ukakanaswa mwenyewe, upanue ujuzi, tajriba na fikara yako, kwani u bado mtovu wa maarifa].

**Kauli yake**: Nathibitisha kauli tatu za uongo waziwazi ambazo si kazi ya mtu yeyote mwenye imani bali yule ambaye anayo haya hata kidogo sana.

**Nasema**: Ee mtovu wa haya, sihuzunikii kauli yako hii pia hata kidogo kwani umetimiza desturi na ada ya wasio na imani wa zamani. Kila Nabii, Mtume wa Mungu, mkweli na *Siddiki* aliyekuja duniani, makafiri wenye bahati mbaya wakamwita mwongo, bali wakamwita kadhabu. Nawe kwa hujudi yako yote umetoa sehemu tatu ambapo kwa mawazo yako batili nimesema uongo, na sehemu zile tatu ni hizi ninazojibu:

**Kauli yake**: Uongo wa kwanza ni huu kwamba kwenye uk. 5, mistari 20-21 imeandikwa: kwa kuwa katika Kurani Tukufu kusema لَمَّا تَوَفَّيْتَنِيْ na katika Hadithi kama ilivyo katika Bukhari, kueleza maana yake اَمَتَّنِيْ [Uliponifisha].

**Nasema**: Muhtasari wa ibara mbovu hii na ya upuuzi ya huyu mpinzani mpumbavu ni huu kwamba katika Sahihi Bukhari katika sehemu hiyo katika tafsiri ya aya يٰعِيْسٰٓى اِنِّىْ مُتَوَفِّيْكَ kuna kauli hii: مُتَوَفِّيْكَ مُمِيْتُكَ , yaani maana ya مُتَوَفِّيْكَ ni مُمِيْتُكَ, siyo kauli hii: لَمَّا تَوَفَّيْتَنِيْ ۔ اَمَتَّنِيْ. Jibu lake ni kwamba hapo kusudio la kauli yangu ni kueleza

kimuhtasari muradi wa Hadithi, siyo kuandika maneno hasa ya Hadithi fulani, kama vile kwa kueleza sentensi yangu hii kwamba 'Na katika Hadithi zingine kama vile katika Bukhari na kadhalika.' Lengo langu hili linafahamika, na mwadhilifu kwa kutafakari maneno yangu hatabaki na shaka kwamba hapa lengo langu ni kuandika muhtasari wa Hadithi zile na muradi wa kauli hizo, sio kunakili ibara. Na ni dhahiri kwamba mtu ambaye, kwa mfano, anaanza kueleza maana ya Hadithi ishirini zenye maneno mbalimbali na muradi wao ni mmoja, basi analazimika kuandika neno lililo kiini cha Hadithi zile ili neno lile lifae kwa hizo zote. Na vile vile lieleze kusudio lenyewe. Hivyo, kusudio hasa la Bukhari na vinginevyo ni اَمَتَّنِیۡ [Uliponifisha] lililopaswa kutajwa. Na ingawa maneno hasa ya Bukhari ni مُتَوَفِّيۡكَ مُمِيۡتُكَ , lakini katika maelezo yangu maneno ya Bukhari tu hayakulengwa, bali ni mazungumzo kwa ujumla juu ya Hadithi iwe katika Bukhari au minghairi ya Bukhari. Tena hii pia ni dhahiri kwamba Bwana Bukhari mwenyewe amehakikisha hapo aya hii, yaani فَلَمَّا تَوَفَّيۡتَنِیۡ – akitaja kusaidiana kwa aya mbili – kwamba hiyo ndiyo maana ya فَلَمَّا تَوَفَّيۡتَنِیۡ , na hapo maana ile aliyoeleza Ibn Abbas ni sahihi kama ilivyo sahihi katika اِنِّیۡ مُتَوَفِّيۡكَ . Aidha hapa hii pia ikumbukwe kwamba Mwenyezi Mungu aliye Mkweli wa wakweli, Amegawanya ukweli katika Neno Lake kwa namna mbili. Ukweli mmoja ni kuhusiana na kauli kidhahiri na wa pili, kuhusiana na maelezo na natija. Mfano wa ukweli wa aina ya kwanza

ni huu kama Mwenyezi Mungu Akasema Isa[as] alikuwa mwana wa Mariamu, na Ibrahimu alikuwa na wana wawili Ismaili na Isihaka; kwani matukio ya kidhahiri bila maelezo ni hayo tu. Na mfano wa ukweli wa aina ya pili ni kama katika Kurani Tukufu maneno ya makafiri au waaminio wa zamani yametajwa kwa mabadiliko kidogo, na ikasemwa kwamba hayo ni maneno yao; au visa vya Torati vilivyoelezwa na humo kuna mabadiliko makubwa. Kwani, ni dhahiri kwamba jinsi zilivyo ibara za Kurani kwa namna ya kimuujiza na sentensi zenye ufasaha na istiara za kuvutia, kauli zenye ufasaha kama hizo zilikuwa hazikutoka kamwe vinywani mwa makafiri wala haukuwa mpangilio huu, bali mpangilio huu wa visa uliomo katika Kurani haumo kamwe katika Torati pia, ilihali Amesema إِنَّ هٰذَا لَفِي الصُّحُفِ الْأُولٰى صُحُفِ إِبْرٰهِيمَ وَمُوسٰى[22] .

Na kwa maneno haya, kwa sura yao, mpangilio wao na njeo zao ni yale yale yaliyotoka kwa mfano vinywani mwa makafiri, basi kwa sababu ya hayo muujiza wa Kurani unabatilika. Kwani, katika hali hii ufasaha ule ukawa wa makafiri sio wa Kurani. Na kama siyo yale yale, basi kwa kauli yako hayo yamelazimika kuwa uongo. Kwani, watu hao walitumia maneno, mpangilio na njeo tofauti. Na kwa vile مُتَوَفِّيكَ na مُمِيتُكَ zilivyo njeo mbili tofauti, hivyo ndivyo kwenye mamia ya sehemu njeo zao na njeo za Kurani zilivyotofautiana. Mathalani,

[22] Al-A'lla, 87:19-20

katika Torati kuna kisa cha Yusuf[as], fungua Torati ukakisome, kisha ukilinganishe na Sura Yusuf ya Kurani Tukufu na uone kwamba kuna tofauti kiasi gani ya njeo na mapunguo na mazidio katika maelezo, bali katika baadhi ya sehemu kidhahiri kuna hitilafu ya maana pia. Kadhalika Kurani Tukufu imeeleza kwamba baba ya Ibrahimu alikuwa Azar, lakini mufasirini wengi wanaandika kwamba baba yake alikuwa mwingine, si Azar. Ewe mjinga, sasa tubu haraka kwamba umeishambulia Kurani kama mapadri. Hadithi ya kwanza katika Sahihi Bukhari ni إِنَّمَا الْأَعْمَالُ بِالنِّيَّاتِ [amali huzitegemewa nia]. Basi, tulipoona kwamba hapa kusudio moja la Hadithi zote ni kwamba maana ya تَوَفَّيْتَنِي ni أَمَتَّنِي , basi kwa nia safi tukaitaja. Maelezo ya aina hii yanahusianaje na uongo, na uongo unayahusuje. Je hii si kweli kwamba shabaha ya Imamu Bukahri kwa sentensi hii مُتَوَفِّيكَ مُمِيتُكَ ni kuthibitisha kwamba maana ya فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي ndiyo أَمَتَّنِي . Kwa hiyo akitaja katika sehemu moja aya mbili za sehemu mbili mbalimbali na akitilia nguvu kwa kuonyesha hizo mbili zinasaidiana Bwana Bukhari anataka kueleza kuwa kusudio la Ibn Abbas lilikuwa hili kwamba maana ya لَمَّا تَوَفَّيْتَنِي ni أَمَتَّنِي. Kwa hiyo sisi pia kimaelezo na kimatokeo tukasema kwamba sawa na Hadithi maana ya لَمَّاتَوَفَّيْتَنِي ni أَمَتَّنِي [uliponifisha].[23] Ebu,

[23] Mamia ya kauli kama hizi zimo katika Kurani Tukufu kwamba maneno ya mzungumzaji yalikuwa mengine na namna tofauti, lakini Mwenyezi Mungu Akaeleza kwa namna nyingine, na kisha

ikiwa hii siyo sahihi, basi sema kwamba ambapo maana ya تَوَفَّيْتَنِىْ ndiyo مُمِيْتُكَ , basi sawa na kauli hii ya Ibn Abbas[ra] لَمَّا تَوَفَّيْتَنِىْ itakuwa na maana gani? Je haitulazimu kwamba tufasiri لَمَّا تَوَفَّيْتَنِىْ sawa na Hadithi, kama vile sawa na Hadithi لَمَّا تَوَفَّيْتَنِىْ ikafasiriwa. Kama tunaruhusiwa kwamba katika tafsiri ya aya mbili za aina moja tutoe kama hoja tafsiri ya aya moja, basi kuna uongo gani kwamba tuliandika ya kuwa sawa na Hadithi maana ya لَمَّا تَوَفَّيْتَنِىْ ni اَمَتَّنِىْ . Ambapo njeo moja ya ***Tawafii*** sawa na Hadithi, imepatikana na maana ya kufisha, basi kwa nini kutumia maana hiyo hiyo katika njeo nyingine inafahamika kuwa nje ya muradi wa Hadithi na kusema kwamba tutaiita kauli ile tu kuwa Hadithi ambayo ***isnad***[24] yake inamfikia Mtume[saw] – yaani iwe ***Marfuu Muttasil***, ni ujahili mwingine. Je Hadithi ambayo ***isnad*** yake imekatika na haimfikii Mtume[saw] haiitwi Hadithi? Maimamu na muhaddithina wa dhehebu la Shia hawafikishi Hadithi yoyote mpaka Mtume[saw], basi je habari zile hawaziiti Hadithi? Na mhadithina na Masuni wakiita baadhi ya habari kuwa ***Maudhuu'*** (ya kutungwa), wameziita Hadithi. Na wakigawanya Hadithi katika aina kadhaa, wakaziita zote kuwa Hadithi. Ni masikitiko

---

Akasema, hii ni kauli yake. Ni masikitiko kwamba kwa sababu ya ubahili dhidi yangu watu hao sasa wameanza kuipinga Kurani Tukufu pia. Sasa alama za kutisha zimedhihirika, Mungu Arehemu. Amin. Mwandishi.

[24] ***Isnad*** ni mnyororo wa wasimulizi wa Hadithi. Mwenezi

kwamba hali yenu imeharibika kiasi hiki kwamba mnaiita njia ile kuwa uongo, ambayo Kurani imeifuata, na kwa shari mnalishambulia neno Takatifu la Mungu. Ni dhahiri kwamba, mathalani, akisema kwamba nimekula sahani nzima ya pilau, basi hatuwezi kusema amesema uongo – uongo huu kwamba amekula pilau, hakula sahani, kwa kuivunja nususi za Hadithi zitumikapo kwa jumla, basi kusema kwamba sawa na Hadithi maana ya لَمَّا تَوَفَّيْتَنِىْ ni اَمَتَّنِى , yaani kwa sababu hii kwamba imeshatumika tayari مُتَوَفِّيْكَ مُمِيْتُكَ , kuna uongo gani humo. Lakini nani amfahamishe mjinga wa namna hii ambaye ujahili wake umechanganyika na sumu ya uadui pia. Lakini ni afadhali kwamba kama vile watu hao wanavyomnasibishia Hadhrat Ibrahim[as] kauli tatu za uongo ndivyo wakaninasibishia pia kauli tatu za uongo. Tunaona fahari kushabihiana na Ibrahimu, lakini twawatupia usoni mwao uongo na uzushi wa watu hao.

**Kauli yake**: Uongo wa pili umeandikwa kwenye ukurasa huo katika mistari 23, 24. Kauli hii ya Kurani Tukufu kwamba kabla ya Mtume Mtukufu[saw] hakuna Nabii ambaye hajafa, pia ni uongu mtupu. Ndani ya Kurani Tukufu imo hii tu: قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ , ambayo maana yake ni hii kwamba Mitume walipita kabla ya Mtume[saw] wa Mungu.

**Nasema**: Je kupita ni kitu kingine minghairi ya kufa? Mtu aliyeaga dunia, huyo tu ndiye anaitwa amekufa. Sheikh Sa‘di amesema:

Baba yangu alipokaribia kumaliza umri wake akanisihi hivi na akapita dunia.[25]

Sasa sema, hapa بگذشت (kapita) yamaanisha nini? Je baba yake Sheikh Sa‘di[rha] alikwenda mbinguni pamoja na mwili wake au alikufa. Ee azizi, je kwa maelezo haya mabovu itathibitika kwamba Hadhrat Isa[as] alikwenda mbinguni kwa mwili wake. Ni usemi wa dunia nzima kwamba, mathalani, inaposemwa mgonjwa fulani ameiaga dunia, kauli hii haimaanishi kwamba amepaa mbinguni na mwili wake. Hata kwa Kiarabu pia maana ya kupita kuwa kufa ni usemi wa zamani. Kuhusu mtaalamu fulani aliyetaka kuandika kitabu fulani, lakini akafa kabla ya kuandika, kuna ubeti huu wa zamani wa mtu fulani:

وَ لَمْ يَتَّفِقْ حَتّٰى مَضٰى بِسَبِيْلِهٖ وَ كَمْ حَسَرَاتٍ فِيْ بُطُوْنِ الْمَقَابِرِ

Yaani, mtaalamu huyu alikuwa hajapata kuandika kitabu mpaka akapita dunia; na kuna majuto mengi katika tumboni mwa makaburi. Yaani, watu wengi wanakufa kabla ya kutimiza nia zao na wanaenda makaburni kwa majuto. Sasa angalia, hapa pia kupita kumetumika kwa

[25] Tafsiri ya ubeti wa Kiajemi

maana ya kufa. Na ukisema mfasiri gani ameandika maana hii, basi jibu lake ni kwamba kila mfasiri mhakiki mwenye akili na busara na mwenye hadhi katika ujuzi wa busara anaandika maana hii tu. Tazama ***Tafsir Madh'harii*** uk. 485, chini ya aya قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ , yaani مَضَتْ وَ مَاتَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ , yaani Manabii wa zamani wameshapita dunia na kufa; na الف لام (Alif na Lam) yaashiria kwamba miongoni mwao hakuna aliyesalimika kufa. Kadhalika katika ***Tafsiri Tabsirur Rahman wa Taisirul Mannan*** ya Sheikh Allama Zainud-Din Ali Al-Muhaaimii, chini ya aya قَدْ خَلَتْ , imeandikwa: مِنْهُمْ مَنْ مَاتَ وَ مِنْهُمْ مَنْ قُتِلَ فَلَا مَنَافَاتٍ بَيْنَ الرِّسَالَةِ وَالْقَتْلِ وَ الْمَوْتِ . Tazama uk. 177, jalada la kwanza la ***Tabsirur Rahman.*** Yaani, manabii wa zamani wamepita dunia hivi kwamba mwingine alikufa na mwingine aliuawa; basi hakuna pingamizi baina ya unabii na mauti na kuuawa. Vilevile tafsiri ***Jaami'ul Bayan*** ya Sheikh Allama Seyid Mu'inud Din bin Sheikh Seyid Safiyyud Din kwenye uk. 21 chini ya aya قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ imeandikwa kwamba قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلِ بِالْمَوْتِ اَوِالْقَتْلِ فَيَخْلُوْ مُحَمَّدٌ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ اَيْضًا , yaani Manabii wote waliokuwa kabla ya Mtume[saw] walipita dunia kwa kufariki au kuuawa; basi Mtume Mtukufu[saw] pia atapita dunia. Kadhalika katika ***Hashia Ghaayatul Kadhi wa Kifaayatur Radhi 'Alaa Tafsiril Baidhawi,*** J. 3, uk. 68 kuhusu sehemu hiyo iliyotajwa juu imeandikwa: لَيْسَ (رَسُوْلُنَا صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) مُتَبَرَّءً عَنِ الْهَلَاكِ كَسَائِرِ الرُّسُلِ وَ يَخْلُوْ كَمَا خَلَوْا . Yaani, Mtume wetu[saw] hakutengwa na kufa, bali

kama vile Mitume wote wa kabla yake walivyofariki, yeye pia atakufa; na kama hao wakapita dunia, yeye pia atapita. Vilevile katika *Tafsir Jaml* ambayo jina lake la pili ni *Futuhati Ilahiyya*, J 1, uk. 336, chini ya aya وَمَا مُحَمَّدٌ... قَدْ خَلَتْ imeandikwa hii كَاَنَّهُمْ اعْتَقَدُوْا اَنَّهُ لَيْسَ كَسَائِرِ الرُّسُلِ فِيْ اَنَّهُ يَمُوْتُ كَمَا مَاتُوْا , yaani baadhi ya Masahaba walidhani kwamba Mtume[saw] hatakufa kama Manabii wengine, bali atabaki hai, kwa hiyo Akasema, yeye pia atakufa kama walivyokufa Manabii wote wa zamani. Vilevile katika *Tafsir Safi*, chini ya aya iliyotajwa, J. 1, imeandikwa: فَسَيَخْلُوْ كَمَا خَلَوْا بِالْمَوْتِ اَوِ الْقَتْلِ , yaani Hadhrat Seyidna Muhammad[saw] pia atapita duniani kama vile Manabii wengine wakapita dunia kwa kifo cha kawaida au kwa kuuawa. Sasa ni dhahiri kwamba mufasirina hao wote wamefasiri neno خَلَتْ kama مَاتَتْ ; yaani wamefasiri aya hii kwamba kama vile Manabii wote wa zamani walivyokufa, ndivyo hivyo Mtume Mtukufu[saw] pia atakavyofariki. Sasa angalia kwamba juu ya kifo cha Hadhrat Masihi[as], huu ni uthibitisho wazi sana namna gani wanaoeleza mufasirina wote kwa sauti moja kwamba Manabii wote, waliokuja duniani hapo kabla, wote wameshafariki. Isitoshe, ni jukumu la kila mwamino kwamba katika sehemu hii maana, ambayo Mungu Mwenye shani kuu Mwenyewe Ameashiria, afahamu maana hii hii kuwa sahihi na awe na yakini kwamba maana iliyo kinyume chake ni kwenda kombo na kumkana Mungu. Na jambo hili ni wazi sana

bali inang'aa kuliko jua kwamba Mungu Jalali katika tafsiri ya aya: قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ[26] Mwenyewe Amesema kwamba اَفَاْئِنْ مَّاتَ اَوْ قُتِلَ[27] . Basi, aya nzima yamaanisha kwamba Mitume wote wa zamani wameshapita dunia hii kwa kufa au kuuawa. Basi, ikiwa Nabii huyu pia, kama hao, apite kwa kufa au kuuawa, je mtaiacha dini. Hapa jambo hili muhimu linapaswa kukumbukwa kwamba katika sehemu hii Mwenyezi Mungu Amebainisha njia mbili tu za kupita dunia hii. Mosi, kwa njia ya mauti, حَتْفَ اَنْفٍ , yaani mtu afe kifo cha kawaida; na ya pili, auawe. Ilmuradi, Mwenyezi Mungu Amehusuru neno خَلَتْ ndani ya kufa au kuuawa. Basi, ni dhahiri kwamba ikiwa ingekuwa katika elimu ya Mwenyezi Mungu maana ya tatu pia, basi kwa kukamilisha maana za خَلَتْ , angeieleza pia. Kwa mfano angesema اَفَائِنْ مَّاتَ اَوْ قُتِلَ اَوْ رُفِعَ اِلَى السَّمَاءِ بِجِسْمِهٖ كَمَا رُفِعَ عِيْسَى انْقَلَبْتُمْ عَلٰى اَعْقَابِكُمْ , ambayo tafsiri yake ni kwamba Mitume wote kabla yake wameshapita, basi ikiwa Nabii huyu pia afe au auawe au kama Isa[as] apazwe mbinguni kwa mwili kama Isa[as], basi je mtaiondoka dini hii. Ee azizi, sasa, je utampinga Mungu kwamba Akasahau kutaja njia hii ya tatu na kutaja njia mbili tu. Lakini wenye akili wanajua vizuri kwamba neno خَلَتْ lililohitaji kuelezwa, kulieleza

---

[26] Aali 'Imraan 3:145

[27] Aali 'Imraan 3:145

kwa kufa au kuuawa ni dalili mkataa juu ya jambo hili kwamba kwa Mwenyezi Mungu hapa maana ya خَلَتْ ndiyo mauti au kuuawa sio nyingine na hili ni jambo la yakini ambalo kulikataa ni kama kutoka katika utii wa Mungu na kumzulia uongo. Na Mwenyezi Mungu Mwenyewe alipoeleza katika aya hii kwamba maana ya خَلَتْ ndiyo kufa au kuuawa, basi kusema kinyume chake ni uongo adhimu na uzushi mkubwa na sio katika dhambi ndogo bali ni dhambi kabiri. Basi, ambapo kwa Mwenyezi Mungu maana za خَلَتْ ni mbili tu, yaani kufa na kuuawa, basi kuna uzushi na uongu upi utakaokuwa mkubwa zaidi kuliko huu kwamba kama vile Wakristo walivyomwita Hadhrat Isa[as] kuwa mwana wa Mungu bila sababu, hivyo ndivyo, bila sababu na bila dalili na pasipo hoja bayana, iingizwe katika maana ya خَلَتْ kuinuliwa mbinguni pamoja na mwili. Naam, hapa swali litazuka kwamba maimamu wa lugha ya Kiarabu pia wasipokuandika popote maana ya خَلَتْ kwamba mtu aende mbinguni pamoja na mwili, basi kulikuwa na haja gani kwamba Mwenyezi Mungu Akaeleza neno خَلَتْ kwa اَفَاۡئِنْ مَّاتَ اَوْ قُتِلَ . Basi jibu lake ni kwamba Mwenyezi Mungu Alijua kwamba katika zama za upotevu neno خَلَتْ litafasiriwa pia kwamba Hadhrat Masihi[as] amefikishwa mbinguni mzima-mzima pamoja na mwili wake. Kwa hiyo, kwa maelzo haya, Akichukua mapema hatua ya kukinga akakatalia mbali mawazo haya mabovu. Sasa,

kwa utafiti huu wote, unaweza kufahamu kwamba kwa kutoa maana hii sikusema uongo wowote, bali usikasirike, wewe mwenyewe, kwa kutupilia mbali maana ya Kurani, umetumia kauli makuruhi na uongo. Nipo tayari kukupa rupia elfu moja kama zawadi ikiwa uweze kuthibitisha kutokana na aya yoyote ya Kurani Tukufu au Hadithi madhubuti au dhaifu au iliyobuniwa, au kauli yoyote ya Sahaba au ya Imamu mwingine, au kwa hotuba za zama za Ujahili au diwani za zama hizo, au kwa beti za aina zote au kwa nudhumu au nathari yoyote ya wataalamu wa Kiislamu, kwamba maana ya خَلَتْ ni hii pia kwamba mtu aende mbinguni kwa mwili wake. Kutaja خَلَتْ katika Kurani Tukufu kwanza, kisha katika ibara iliyopo kama tafsiri sawa na kanuni ya balagha na semantiki, kutaja kufa au kuuawa, je kwa mwamini hii si hoja mkataa juu ya kwamba hapo maana ya خَلَتْ ni mbili tu, yaani kufa au kuuawa. Sasa baada ya ushahidi wa Mungu kuna haja ya ushahidi wa nani? Alhamdulillahi, tena alhamdulillahi, kwamba katika sehemu hii hii Mwenyezi Mungu ametoa ushahidi wa ukweli wangu na akasema maana ya خَلَتْ ndiyo kufa au kuuawa. Kuhusu habari hii, katika kipeperushi chako umeandika ibara hii dhidi yangu kwamba 'amesema uongo ambao si kazi ya mtu mwaninifu, bali mwenye haya hata kidogo sana.' Lakini, hii pia ni ishara adhimu ya Mwenyezi Mungu kwamba uongo huo umethibitika

dhidi yako kwa ushahidi wa Kurani. Sasa sema nikuambieje? Kwa haraka bila haki wewe uliniita mwongo, lakini sitaki nijibu ubaya kwa ubaya; bali kama katika sheria ya Kiislamu kusema uongo isingekuwa haramu na dhambi, kwa kukulipia kuniita mwongo ningekuita mkweli sana; na kwa kukulipia kuniita kwa uwongo dhalili na mshinde, ningekuita mheshimiwa na mshindi.

**Kauli yake**: Uongo wa tatu, kwenye mstari 27 wa ukurasa huo, kuwa na ijima ya Masahaba[ra] wote juu ya kifo cha Manabii wote, huu pia ni uongo mtupu. Masahaba watakatifu walikuwa zaidi ya laki moja, kuleta uthibitisho wa hao wote ni vigumu.

**Nasema**: Sehemu hii nasikitikia hali yenu kwamba namna gani Mungu aliwaondoleeni mbali akili na elimu na uaminifu vifuani mwenu. Je kwa elimu hii mnaitwa masheikh na kuitana maulamaa wahehimiwa na masufii wenye adhama? Ee jahili mwenye kuhurumiwa, kwa hakika ni kweli kwamba juu ya kifo cha Hadhrat Masihi[as] na ya kifo cha Manabii wote wa zamani ijima ya Masahaba watakatifu ikawa kama vile ikawa ijima ya aina hii hii juu ya Ukhalifa wa Abu Bakr[ra], bali ijima hii ilikuwa bora zaidi kuliko ijima juu ya Ukhalifa wa Abu Bakr[ra]. Na kama inahojiwa ijima hii, basi ijima juu ya ukhalifa huo itahojiwa zaidi sana. Kwa hakika ijima hii ni kubwa zaidi kuliko ijima juu ya Ukhalifa wa Hadhrat

Abu Bakr[ra]. Kwani, hamna hata kauli moja dhaifu pia kuthibitisha kuwa hata Sahaba mmoja akampinga Hadhrat Abu Bakr[ra] au akabaki nyuma. Yaani, kwa kutoa hoja juu ya kifo cha Mtume[saw], Hadhrat Abu Bakr[ra] aliposoma aya hii مَا مُحَمَّدٌ اِلَّا رَسُوْلٌ ۚ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ ۭ اَفَا۟ىِٕنْ مَّاتَ اَوْ قُتِلَ انْقَلَبْتُمْ عَلٰٓى اَعْقَابِكُمْ[28] – ambayo tafsiri yake ni kwamba Muhammad[saw] ni Mtume tu, hana sehemu yoyote ya uungu, na Mitume wote wa kabla yake wameshapita dunia, yaani wameshafariki. Basi, na huyu pia akifariki au akiuawa akapita dunia, je mtaiacha dini? – hapo baada ya kusikiliza aya hii hata Sahaba mmoja hakupinga wala hakuinuka kusema kwamba maelezo yako haya ni nakisi na siyo kamili. Je hujui kwamba baadhi ya Manabii wapo wazima ardhini pamoja na mwili, kama vile Ilyasa na Khadhir, na baadhi yao wapo mbinguni kama vile Idrisa na Isa, basi kwa aya hii chathibitikaje lazima kifo cha Mtume Mtukufu[saw] na kwa nini haijuzu kwamba yeye naye yu mzima. Bali, Mashaba wote wakisikia aya hii wakasadikisha na wote wakafahamu kwamba kama Manabii wote, Mtume Mtukufu[saw] pia alilazimika kufariki. Ijima hii ikatokea papo hapo pasipo kusita. Lakini kuhusu ijima ile inavyokubalika juu ya Ukhalifa wa Hadhrat Abu Bakr[ra], baadhi ya Masahaba wakangoja kidogo na kusita pia,

[28] Aali 'Imraan 3:145

ingawa baada siku chache wakafanya baiati. Na katika jaribio hilo, Hadhrat Ali[ra] mwenyewe pia akaathirika. Lakini, juu ya kifo cha manabii wa zamani, hata Sahaba mmoja baada ya kusikiliza hotuba ya Hadhrat Abu Bakr Siddik[ra], hakupatwa na jaribio wala hakuchelewa wala kusita, bali wote wakaamini mara baada ya kusikia. Kwa hiyo, hii ni ijima ya kwanza katika Islam iliyofanyika pasipo kusita. Muhtasari wa mazungumzo ni kwamba bila shaka sawa na nususi zilizo wazi, itikadi yetu ni hii kwamba ikawa ijima ya Masahaba juu ya kifo cha Manabii wote wa zamani, Hadhrat Masihi[as] akiwa mmoja wao, bali Hadhrat Masihi[as] alikuwa ni lengo la kwanza la ijima hiyo. Sasa, hapa chini naandika sawa na nususi za Hadithi ili ijulikane nani kati yetu sisi wawili ameimarika juu ya ukweli akimcha Mwenyezi Mungu na nani anajasiri kusema uongo na kutengana na nususi zilizo wazi.

Ibainike kwamba kuhusu habari hii, ndani ya Sahihi Bukhari kinachoitwa sahihi sana kuliko vitabu vyote kuna ibara zifuatazo: عَنْ عَبْدِ اللّٰهِ بْنِ عَبَّاسٍ اَنَّ اَبَابَكْرٍ خَرَجَ وَ عُمَرُ يُكَلِّمُ النَّاسَ فَقَالَ اجْلِسْ يَا عُمَرُ فَاَبٰى عُمَرُ اَنْ يَّجْلِسَ فَاَقْبَلَ النَّاسُ اِلَيْهِ وَ تَرَكُوْا عُمَرَ فَقَالَ اَبُوْبَكْرٍ اَمَّا بَعْدُ مَنْ مِنْكُمْ يَعْبُدُ مُحَمَّدًا فَاِنَّ مُحَمَّدًا قَدْ مَاتَ وَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ يَعْبُدُ اللّٰهَ فَاِنَّ اللّٰهَ حَيٌّ لَا يَمُوْتُ قَالَ اللّٰهُ وَ مَا مُحَمَّدٌ اِلَّا رَسُوْلٌ ۚ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ ... اِلَى الشَّاكِرِيْنَ[29]. وَ قَالَ وَاللّٰهِ كَاَنَّ النَّاسَ لَمْ يَعْلَمُوْا اَنَّ اللّٰهَ اَنْزَلَ هٰذِهِ الْاٰيَةَ حَتّٰى تَلَاهَا اَبُوْبَكْرٍ فَتَلَقَّاهَا النَّاسُ كُلُّهُمْ فَمَا اَسْمَعُ بَشَرًا مِنَ

[29] Aali 'Imraan 3:145

النَّاسِ اِلَّا يَتْلُوْهَا ... اَنَّ عُمَرًا قَالَ وَاللهِ مَا هُوَ اِلَّا اَنْ سَمِعْتُ اَبَا بَكْرٍ تَلَاهَا فَعَقَرْتُ حَتّٰى مَا يُقِلُّنِىْ
رِجْلَاىَ وَ حَتّٰى اَهْوَيْتُ اِلَى الْاَرْضِ حَتّٰى سَمِعْتُهُ تَلَاهَا اَنَّ النَّبِىَّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَدْ مَاتَ .

Yaani, Ibn Abbas[ra] anasimulia kwamba Abu Bakr[ra] alitoka (yaani, siku aliyofariki Mtume[saw]) ilhali Umar[ra] alikuwa akiongea na watu (yaani, alikuwa akisema kwamba Mtume[saw] hakufa bali yu mzima). Basi, Abu Bakr[ra] akasema, Ee Umar, keti; lakini Umar[ra] akakataa kuketi. Hapo watu wakamwelekea Abu Bakr[ra] na kumwacha Umar[ra]. Basi, Abu Bakr[ra] akasema, baada ya kumsifu Mungu na kumsalia Mtume[saw], ibainike kwamba miongoni mwenu anayemwabudu Muhammad[saw] ajue kwamba Muhammad[saw] ameshafariki; na anayemwabudu Mungu, basi Mungu Yu Mzima Ambaye Hatakufa. Na ushahidi juu ya kifo cha Mtume[saw] ndio huu kwamba Mungu Alisema, Muhammad siye ila ni Mtume tu, na Mitume wote waliokuwa kabla yake wameshapita duniani, yaani wameshafariki; na Abu Bakr[ra] akasoma aya hii mpaka الشّٰكِرِيْنَ[30]. Msimulizi akasema, Wallahi,

---

[30] Sentensi ya baada ya aya hii اَفَاۡئِنْ مَّاتَ اَوْ قُتِلَ inaeleza wazi kwamba kwa Mwenyezi Mungu kupita kuna aina mbili, kwa njia ya kifo cha kawaida au kwa kuuawa. Na Mwenyezi Mungu hakusema katika aya hii kwamba kupita inakuwa kwa njia hii pia kwamba mtu aende mbinguni mzima kwa mwili wake. Sasa Mwenyezi Mungu Alipoishaeleza kupita kwa maneno اَفَاۡئِنْ مَّاتَ اَوْ قُتِلَ na ameimaliza hapa, basi kutokubali baada ya hapo si kitendo cha mwaminio mwema. Mwandishi

kana kwamba watu hawakuwa na habari hii kwamba aya hii pia Mwenyezi Mungu Ameshusha, na Abu Bakr[ra] alipoisoma watu wakaijua. Basi, Masahaba wote wakajifunza aya hii kutoka kwa Abu Bakr[ra], na hakubaki Sahaba au asiyekuwa Sahaba ambaye alikuwa hasomi aya hii. Na Umar[ra] akasema, Wallahi, nikasikia aya hii kutoka kwa Abu Bakr[ra] tu alipoisoma. Basi, kwa kusikiliza nikapotewa na fahamu na kuumia hata kwamba miguu yangu haikuweza kunibeba na ninaanguka-anguka tangu niliposikia aya hii akiisoma na kusikia akinena maneno haya kwamba Mtume[saw] ameshafariki. Na hapa ipo ibara hii ya Kastalani, sherehe ya Bukhari: وَ عُمَرُ بْنُ الْخَطَابِ يُكَلِّمُ النَّاسَ يَقُوْلُ لَهُمْ مَا مَاتَ رَسُوْلُ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ... وَلَا يَمُوْتُ حَتّٰى يَقْتِلَ الْمُنَافِقِيْنَ . Yaani, Hadhrat Umar[ra] alikuwa akiongea na watu na kusema kwamba Mtume[saw] hakufa wala hatakufa mpaka awaue wanafiki. Na katika *Al-Milal wa An-Nihal* ya Shahristani[31] kuna ibara hii kuhusu habari hii: قَالَ عُمَرُ بْنُ الْخَطَّابِ مَنْ قَالَ اِنَّ مُحَمَّدًا مَاتَ فَقَتَلْتُهُ بِسَيْفِيْ هٰذَا ـ وَاِنَّمَا رُفِعَ اِلَى السَّمَاءِ كَمَا رُفِعَ عِيْسٰى ابْنُ مَرْيَمَ عَلَيْهِ السَّلَامُ وَ قَالَ اَبُوْبَكْرِ بْنُ قُحَافَةَ مَنْ كَانَ يَعْبُدُ مُحَمَّدًا فَاِنَّ مُحَمَّدًا قَدْ مَاتَ وَمَنْ كَانَ يَعْبُدُ اِلٰهَ مُحَمَّدٍ فَاِنَّهُ حَيٌّ لَا يَمُوْتُ وَقَرَءَ هٰذِهِ الْاٰيَةَ وَمَا مُحَمَّدٌ

[31] *Al-Milal* ni ya Abul Fat'h Al-Imam Muhammad ibn Abdul Karim Shahristanii aliyefariki mwaka 548 Hijra. At-Taj As-Subki amesema katika *Tabakaat* yake kwamba kwangu mimi kitabu *Al-Milal wa An-Nihal* cha Shahristani ni kitabu bora zaidi kuhusu habari hii, uk. 9. Mwandishi

اِلَّا رَسُوۡلٌ ۚ قَدۡ خَلَتۡ مِنۡ قَبۡلِهِ الرُّسُلُ ؕ اَفَا۠ئِنۡ مَّاتَ اَوۡ قُتِلَ انۡقَلَبۡتُمۡ عَلٰۤى اَعۡقَابِكُمۡ [32] فَرَجَعَ الۡقَوۡمُ اِلٰى قَوۡلِهٖ .
Tazameni ***Milal Nihal,*** J. 3. Tafsiri ni hii kwamba Umar Khattab[ra] alisema, mtu atakayesema kwamba Mtume Mtukufu[saw] amefariki, mimi kwa upanga wangu huu nitamwua; bali, amenyanyuliwa mbinguni kama vile Isa bin Mariamu alivyonyanyuliwa. [33] Na Abu Bakr[ra]

---

[32] Aali 'Imraan 3:145

[33] Kwa kauli hii ya Hadhrat Umar[ra] kwamba mtu atakayenena kuhusu Hadhrat Seyidna Muhammad Mteule[saw] kwamba amefariki, nitamwua kwa upanga wangu, inaonekana kwamba Hadhrat Umar[ra], kwa fikara yake fulani akapita kiasi kuhusu uzima wa Mtume Mtukufu[saw] na akaona kusema kwamba Mtume[saw] amefariki na kauli ya kufuru na kuritadi. Mwenyezi Mungu Ampe Hadhrat Abu Bakr[ra] maelfu ya malipo mema kwamba haraka sana akaondoa fitina hii na akitaja nususi bayana akathibitisha kwamba Manabii wote wa zamani wameshafariki. Na kama vile yeye alivyowaua Musailima kadhabu, Aswad 'Ansi na wengineo, kwa kweli kwa maelezo haya pia aliwaua waongo wa zama za upotevu kwa ijima ya masahaba wote kana kwamba si waongo wanne bali akawaua waongo watano. Ee Mungu wangu, ishushie roho yake mamilioni ya rehema. Amin. Sehemu hii kama **خَلَتْ** ifasiriwe kwamba baadhi ya Manabii wameshakwenda mbinguni wazima, basi Hadhrat Umar[ra] anaonekana mkweli na aya hii haimdhuru bali inamwunga mkono. Lakini sentensi iliyo baada ya aya hii itoayo maelezo – yaani اَفَا۠ئِنۡ مَّاتَ اَوۡ قُتِلَ ]Aali 'Imraan 3:145[–ambayo Hadhrat Abu Bakr[ra] akaitupia jicho, hudhihirisha kwamba kufasiri hivi aya hii kwamba Manabii wote walipita, ingawa walipita wakifa au walipita wakiwa hai, ni kulaghai,

akasema, yule anayemwabudu Muhammad[saw] basi huyu lazima ameishafariki, na anayemwabudu Mungu wa Muhammad[saw], basi Yu Mzima, Hatakufa, yaani Mungu pekee tu Anayo sifa hii kwamba Yu Mzima wa milele, na wengine wote wanadamu kwa wanyama hufariki kabla ya kudhaniwa kuishi milele. Kisha, Hadhrat Abu Bakr[ra] akasoma aya hii ambayo tafsiri yake ndiyo hii kwamba Muhammad[saw] ndiye Mtume, na Mitume wote wameshapita duniani. Kama huyu naye akifa au kuuawa, basi je mtaritadi? Ndipo watu wakisikia aya hii wakaachana na mawazo yao. Sasa, tafakari kwamba

---

kugeuza na uzushi adhimu kinyume cha kusudio la Mungu. Na wazushao kusudi ambao hawaogopi siku ya uadilifu na wanafasiri kinyume cha maelezo ya Mungu Mwenyewe, bila shaka hao ndio chini ya laana ya kudumu. Lakini, Hadhrat Umar[ra] hakuwa na elimu mpaka wakati ule na Masahaba wengine pia walikuwa na wazo hilo lisilo sawa na walishikwa na usahaulifu na mghafala unaolazimu ubinadamu na wakafikiri moyoni mwao kwamba baadhi ya Manabii wapo wazima mpaka sasa na watakuja tena duniani, basi kwa nini Mtume Mtukufu[saw] asiwe kama hao. Lakini Hadhrat Abu Bakr[ra] akisoma aya nzima na kuwasomea اَفَاۡىٕنۡ مَّاتَ اَوۡ قُتِلَ akatilia mioyoni kwamba maana ya خَلَتۡ ni ya aina mbili tu. (1) Kifo cha kawaida, (2) Kuuawa. Hapo wapinzani wakakiri kosa lao na Masahaba wote wakaafikiana juu ya kwamba Manabii wote wa zamani wameshafariki na sentensi اَفَاۡىٕنۡ مَّاتَ اَوۡ قُتِلَ ikaleta athari kubwa na wote waakaachana na mawazo ya upinzani. Basi Alhamdulillahi juu yake. Mawandishi

ikiwa Hadhrat Abu Bakr[ra] hakueleza hii kutoka katika Kurani kwamba Manabii wote wameshafariki na pia ikiwa maelezo haya hayakuwa mkataa, basi Masahaba ambao kwa kauli yako walizidi laki moja wakakubalije jambo la dhana na shaka, na kwa nini hawakutoa hoja hii wakisema, Ee mheshimiwa, ushahidi wako huu ni nakisi na hunayo nususi yoyote mkataa. Je hujajua bado kwamba Kurani katika aya رَافِعُكَ اِلَیَّ yaeleza kwenda kwa Hadhrat Masihi[as] mbinguni pamoja na mwili wake. Je hujasikia بَلْ رَّفَعَهُ اللّٰهُ اِلَيْهِ pia? Basi, kwa nini Mtume[saw] kwenda huko mbinguni haiwezekani sawa na maoni yako? Bali, Masahaba wenye ufahamu wa Kurani wakisikia aya na wakikuta tu maelezo ya neno خَلَتْ ndani ya sentensi اَفَاۡئِنْ مَّاتَ اَوْ قُتِلَ[34] mara wakaachana na mawazo yao ya zamani. Naam, mioyo yao ikapatwa na huzuni na kuumia sana kwa sababu ya kifo cha Mtume[saw] na roho yao ikafinywa. Na Hadhrat Umar[ra] akasema kwamba baada ya kusikiliza aya hii, hali yangu ikawa hivi kwamba miguu yangu haiwezi kubeba mwili wangu nami naanguka-anguka chini. Subhanallah, walikuwa wenye bahati nzuri sana namna gani hao na wenye kujitahadhari kuhusu Kurani kwamba baada ya kuzingatia aya walipoelewa kuwa manabii wote wa zamani wameshafariki hawakusema lolote isipokuwa

[34] Aali 'Imraan 3:145

wakaanza kulia na kujaa huzuni; na ndipo Hadhrat Hassaan bin Thabit akatunga wimbo huu wa maziko:

كُنْتَ السَّوَادَ لِنَاظِرِیْ فَعَمِیَ عَلَیْكَ النَّاظِرُ
مَنْ شَاءَ بَعْدَكَ فَلْیَمُتْ فَعَلَیْكَ كُنْتُ اُحَاذِرُ

Yaani, ulikuwa mboni ya jicho langu, basi nimepofuka kwa kufariki kwako. Sasa baada yako wewe niufanyie nini uhai wa mtu yeyote. Isa[as] afe au afe Musa[as]; wafe tu, nilikuwa nakuhuzunikia wewe tu. Ikumbukwe, kama katika mtazamo wa Hadhrat Abu Bakr[ra], Hadhrat Isa[as] angekuwa hajafa, asingetoa kamwe aya hii kama hoja, na kama Masahaba wangekuwa na mashaka kuhusu maana hii ya aya hiyo kwamba Manabii wote wameshafariki, lazima wangesema kwamba kwa kuwa Hadhrat Isa[as] ameishaenda mbinguni akiwa hai, pamoja na mwili wake, basi ushahidi huu si mkamilifu na ipo sababu gani kwamba Mtume Mtukufu[saw] naye pia hakuenda mzima-mzima mbinguni kama Isa[as]. Lakini, ukweli halisi unaoonekana ndio huu kwamba kifo cha Hadhrat Isa[as] nacho kikaamulika siku hiyo hiyo, na Masahaba kwakusikiliza aya hii hawakusema hata kidogo kwamba Hadhrat Isa[as] yu mzima; na kwa kuwa kutokana na neno كُلُّهُمْ la Sahihi Bukhari imethibitika kwamba wakati huo Masahaba wote walikuwepo, na baada ya kusikiliza aya hii mtu yeyote hakupinga, hivyo ikalazimu kukubali kwamba ikapatikana ijima ya hao wote juu ya kifo cha Manabii wote wa zamani; na hii ilikuwa ni ijima ya

kwanza ya Masahaba iliyofanyika. Na ijima hii ilikuwa aula kuliko ijima juu ya Ukhalifa wa Abu Bakr[ra] iliyofanyika baada yake, kwani kuhusu hii mtu yeyote hakusema hata neno moja dhidi yake; lakini kuhusu Ukhalifa wa Abu Bakr[ra] mwanzoni hitilafu ilitokea. Naam, hapa wazo hili linazuka kwamba kabla ya kusikia aya hii, Hadhrat Umar[ra] alikuwa na imani hii kuhusu Hadhrat Isa[as] kwamba licha ya kufa yeye pia atarudi duniani, kwani alishabihisha kunyanyuliwa kwake na kunyanyuliwa kwa Mtume[saw] na alijua kwamba mwili wa Mtume[saw] upo mpaka sasa nyumbani mwa Hadhrat Aisha[ra], basi juu ya kukiri kushabihiana kivipi angeweza kukubali kwamba mwili wa Hadhrat Masihi[as] ulikwenda mbinguni. Lakini, akisikiliza aya akaachana na wazo hili pia, na siku ile Masahaba wote wakaamini kwamba Manabii wote wa hapo kabla wameshafariki. Na kwa kweli huu ulikuwa utovu wa adabu sana na dhambi kubwa kwamba nabii aliye Khatamur-Rusul na Mbora wa manabii afe, na maiti yake iwe mbele yao na kumhusu Nabii mwingine liwepo wazo kwamba yeye hajafa. Kwa kweli, wazo hili na huba na heshima ya Mtume Mtukufu[saw] haviwezi kujumuika mhali pamoja. Tafakari kwa uaminifu na takwa kwamba kusema kwa Hadhrat Umar[ra] kuwa Mtume Mtukufu[saw] hajafa bali amenyanyuliwa mbinguni kama Hadhrat Isa[as], wazo hili liliwezaje kufutiliwa pasipo Hadhrat Abu Bakr[ra]

kuthibitisha kifo cha Hadhrat Masihi[as] na Manabii wote wa zamani? Ebu, kama Hadhrat Abu Bakr[ra] hakunuia kusoma aya hii قَدْ خَلَتْ kwa kuthibitisha kifo cha Hadhrat Masihi[as] na Manabii wengine wa zamani, basi akafulilia je wazo la Hadhrat Umar[ra]? Msingi wote wa wazo hili la Hadhrat Umar[ra] ulikuwa juu ya kunyanyuliwa mzima kwa Hadhrat Masihi[as]. Na inaonekana kwamba baadhi ya Masahaba sawa na uelewa wao walifahamu kwamba Hadhrat Isa[as] alikwenda mzima mbinguni na kisha alipofariki Mtume Mtukufu[saw] wazo hili likazuka moyoni mwa Hadhrat Faruk[ra] kwamba kama Hadhrat Masihi[as] ameenda mzima mbinguni, basi Nabii wetu anayo haki zaidi na ni aula kwamba aende mzima mbinguni, kwani hii ni fadhila adhimu kwamba Mwenyezi Mungu Amwite Nabii yeyote mzima kuja kwake huko mbinguni. Na kwa methodolojia na adabu nzuri ilikuwa kama kufuru kufikiri kuwa Hadhrat Masihi[as] alikwenda mzima mbinguni lakini Nabii aliye Khatam wa Manabii na Mbora wa Manabii anayehitajika sana asifikie hata umri wa kawaida. Kama si kutoamini na uadui, aya hii iliyotajwa hapo juu ni nususi kubwa wazi juu ya Masahaba wote kuafikiana kwamba Masihi na Manabii wengine wote wa zamani wameshafariki. Na kama si hivyo, basi ebu, semeni kwa kutumia akili na kumcha Mungu kwamba wakati wa hitilafu iliyotokea baina ya rai ya Hadhrat Abu Bakr[ra] na rai ya Hadhrat Umar[ra],

Hadhrat Umar[ra] alisema kuthibitisha rai yake kwamba Hadhrat Isa[as] alinyanyuliwa mzima mbinguni, basi na Mtume Mtukufu[saw] pia atanyanyuliwa hivyo, kwa nini, basi, ni marufuku na muhali kwamba Mtume Mtukufu[saw] juu ya kuwa mbora na mwenye fadhila asinyanyuliwe mbinguni kama Hadhrat Masihi[as]? Wakati huo aya قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ[35] aliyosoma Hadhrat Abu Bakr[ra] kwa kupinga rai ya Hadhrat Umar[ra], kama hakukusudia kwayo kwamba Hadhrat Isa[as] pia anayetajwa ameshafariki, basi akakusudia nini, na kwa njia gani wazo la Hadhrat Umar[ra] lingeweza kufutiliwa mbali bila hii? Na kusema kwako kwamba haikufanyika ijima juu yake, ni uongo mtupu hata naihuzunukia hali yenu kwamba imefikia wapi. Ee azizi, ndani ya Bukhari, katika sehemu hii kuna neno la كُلُّهُمْ linalodhihirisha kwamba Masahaba wote walikuwepo wakati ule. Na jeshi la Usama la watu elfu ishirini likakoma kuondoka kwa sababu ya msiba huu mkuu wa kifo cha Mbora wa Mitume. Na yu nani mwenye bahati mbaya aliyesikia habari ya kifo cha Mtume[saw] na mara moja hakuhudhiria. Ebu, taja jina la mtu yeyote. Isitoshe, hata kama tukidhani kwamba baadhi ya Masahaba hawakuhudhuria, hao hatimaye baada ya mwezi mmoja, miwili au miezi sita lazima walikuja. Basi, kama

[35] Aali 'Imraan 3:145

walidhihirisha rai tofauti na kutoa maana tofauti ya aya قَدْ خَلَتْ , basi uilete. Na kama usiweze kuleta, basi hii ndiyo kinyume cha imani na uaminifu kwamba unayo itikadi dhidi ya ijima kamili ya namna hii. Hii ni ijima madhubuti juu ya kifo cha Hadhrat Masihi[as] kwamba mtovu wa imani tu anaweza kuikataa, lakini mwenye bahati njema na mcha-Mungu hataikanusha katu. Sasa ijima ilifanyika juu ya kifo cha Hadhrat Masihi[as]; sema juu ya uhai ijima imethibitika wapi? Mufasirina wanaandika kwamba kuna kauli hii pia kwamba Masihi alikufa kwa siku tatu au kwa saa tatu; kana kwamba wanaleta fikara ya vifo viwili kwa Masihi, kifo chake cha kwanza na kifo chake cha pili. Na kuna kauli ya Imam Malik kwamba alikufa kwa kudumu, kauli hiyo hiyo ni ya Imam Ibn Hazm pia. Mu'tazila nao huamini kifo chake barabara. Na baadhi ya makundi ya Masufii wanaamini kwamba Isa Masihi[as] alifariki, na juu ya hulka na sifa zake mtu mwingine atakuja duniani miongoni mwa umati huu na akiwa dhihirisho lake ataitwa Masihi Mau'udi. Sasa tazameni kila mtu ana kauli yake, ijima iko wapi? Ijima ilifanyika juu ya kifo tu, na ijima hiyo ikawahilikisheni. Sasa kama Washia endeleeni kumlaumu Hadhrat Abu Bakr[ra] aliyeng'olea mbali itikadi yenu hii.

اعلموا رحمكم الله ان حاصل كلامنا هذا ان الاجماع على موت المسيح عيسى بن مريم وغيره من النبيين الذين بعثوا قبل سيدنا ورسولنا المصطفى صلى الله عليه وسلم ثابت

متحقق بالنصوص الحديثية القطعية والروايات الصحيحة المتواترة۔ ويعلم كل من عنده علم الحديث ان هذا الاجماع قد انعقد فی ناد محشود و محفل مشهود عند اجتماع جميع بدور الاصحاب وبحور الالباب۔ فما تناضلوا بالانكار۔ وما ردّوا رأی امامهم المختار۔ وما ذكروا شيئا من هفوته۔ وما صالوا علیٰ فوهته۔ بل سكنت عند بيان الصديق قلوبهم۔ ومالت الی السلم حروبهم۔ ووجدوا البرهان المحكم والدليل القویّ الجليل۔ فتحاموا القال والقيل۔ وصُقِلَ الخواطرُ۔ وانار القلوبُ ونشط الفاتر۔ وكانوا قبل ذالك غرضَ اللّظی۔ او كرجل التهبت احشاءه بالطوٰی بما عيل صبرهم بموت النبیّ سيدهم المصطفٰی محمد المجتبیٰ وبما قلقت قلوبهم وصار فؤادهم فارغا بما فقدوا حبّهم خير الوریٰ وكانوا كالمبهوتين فاذا قام عبد الله الصديق۔ فتح عليهم باب التحقيق۔ و اَروَاهُم من هٰذا الرحيق۔ و قُضِیَ الامر واُزيل الشبهاتُ۔ وسكنت الاصواتُ۔ وانعقد الاجماع علیٰ موت المسيح وسائر الانبياء الماضين۔ بل هو اوّل ما اجمع عليه الصحابة بعد موت خاتم النبيين۔ ولهٰذا الاجماع شان اكبر من اجماعٍ انعقد علیٰ خلافة ابی بكر الصديق فانّ الصحابة اتفقوا عليه كلهم وما بقی من فريق۔ وقبلوا ذلك الامر من غير تردّد وتوقفٍ بل بأتمّ الاذعان واليقين۔ وكان كلهم يتلون الآيت ويُقرُّون بموت الرسل ويبكون علی موت سيّد المرسلين۔ حتّی اذا سمع الفاروق الاٰية قال عُقِرت وما تقلنی رجلای وكان من الحزن كالمجانين۔ وقال حسّان وهو يرثی رسُول الله صلّی الله عليه وسلم۔

كُنْتَ السَّوَادَ لِنَاظِرِیْ فَعَمِیَ عَلَيْكَ النَّاظِرُ
مَنْ شَاءَ بَعْدَكَ فَلْيَمُتْ فَعَلَيْكَ كُنْتُ اُحَاذِرُ

يعنی ای سيّدی وحبيبی كنت قرّة عينی فَفَقَدَ نُور عينی بفُقدانك ولا ابالی بعدك ان يموت عيسیٰ او مُوسیٰ اونبی آخر فانی كنت عليك اخاف فاذا متَّ فليمت من كان من السّابقين وفی هٰذه اشارة الی اَنّ الاٰية التی تلاها الصديق نبّهت الصحابة علیٰ موت الانبياء كلهم فما بقی لهم همّ فی شانهم مثقال ذرّة وما كانوا متأسفين۔ بل استبشروا بموت الجميع بعد موت رسُولهم الامين ولو كان الامر خلاف ذلك اعنی ان ثبت حيٰوة احد من الانبياء السابقين بنصّ القرآن وبآية من آيات الفرقان فكادوا ان يموتوا اسفا علی رسولهم وكادوا ان يلحقوا بالميتين۔ ولكنهم لمّا علموا ان رسُولنا صلّی الله عليه وسلّم ليس بمنفرد بورود الموت من

الله العلّام بل الانبياء كلهم ماتوا من قبل وسقوا كأس الحمام تهلّلت وجوههم واستبشرت قلوبهم فكانوا يتلون هٰذه الاٰية فی سکك المدينة واسواقها ومات المنافقون ولم يبق لهم سعة ان يعترضوا على الاسلام بموت نبينا الصبيح وحيات المسيح فالحمد لله علٰى هٰذا العون الصريح۔ ان كلمة الاسلام هى العليا ويبرق نوره من كل جنب وشفا۔ والله ارسل محمّدًا وهويكرمه الى يوم الدين۔ واذا ثبت الاجماع ولم يبق القناع وسطع الصبح وازال الظلمة الشعاع۔ فاسئل المنكرين مابقى من عذرهم وقد حصحص الحقّ النباعُ وكُرّر الثبوتُ واحكمت الاضلاعُ وكمل الادواء والاهجاعُ۔ فمن ادعى بعد ذلك علٰى رفع هذاالاجماع۔ وعزآ امرنا الى الابداع۔ فعليه الدليل القطعى من الكتاب والسنة واثبات اجماع انعقد علٰى حيات المسيح فی عهد الصحابة۔ وانّٰی لهم هٰذا ولو ماتوا متفكرين۔ وكيف وليس عندهم حجة من الله وليس معهم سلطان مبين۔ ان يتبعون الّا آباءهم الذين كانوا مخطئين۔ قست القلوب ورُفعت الامانت وما بقى فيهم الا فضول الهذر وما بقى فيهم من يطلب كالمتقين۔ و اذا قيل لهم آمنوا بمن جائكم من عند ربكم علٰى رأس المائة وعند ضرورةٍ احسّها قلوب المؤمنين۔ قالوا لا نعرف من جاء وما نراه الا احدًا من الدجّالين وقد عُلّموا انّه يجیء هم حكمًا عدلًا ويحكم بينهم فيما كانوا فيه مختلفين۔ فكيف يصير حاكمهم محكومهم وكيف يقبل كلما اجمعوا من رطب و يابس مالهم لا يتفكرون كالعاقلين۔ و يسبّوننى عدوا بغير علم فالله خير محاسبا وهويعلم ما فی صدور العالمين۔ وقد كانوا يستفتحون من قبل ويعدّون المائين۔ فلمّا جاء هم من يرقبونه نبذوا وصايا الله ورسُوله وراء ظهورهم كانه جاء فی غير وقته وكانهم ما عرفوه من علامة وكانوا من المعذورين۔ الم يروا كيف يتم الله به الحجّة بآيات السماء ويعصم عرض رسُوله من قوم كافرين۔ بل كفروا به وقالوا فاسقٌ ومن المفترين۔ فسيعلمون من فسق ومن كان يفترى على الله وان الله لا يخفى عليه خافية والله لا يجعل عاقبة الخير اِلّا لقوم متقين۔ و ما قيل لى الّا ما قيل للرسل من قبل تشابهت القلوب۔ وزُيّن لهم اعمالهم وحسبوا انهم يعطون الثواب على ما يؤذوننى ويدخلون الجنّة بالتحقير والتكذيب والتوهين۔ و كفّرونى وفسّقونى و كذّبونى وجهّلونى وقالوا كافرٌ شرّ النّاس۔ ولوشاء الله لما قالوا ولٰكن ليتمّ ما جاء فی نبأ خير المرسلين۔ ومايٰنطقون الّا بطرًا ورياءَ الناس ولا يدبّرون الاَمْرَ كالمنصفين۔ ولا تجدفی قلوبهم احقاق الحق

كالصالحين بل تجد كثيرا منهم يكيدون كل كيدٍ ليطفؤآ نور الله بافواههم وما كانوا خائفين۔ الا يقرء ون القراٰن اَوْلا يجاوزحناجرهم اوصاروا من المعرضين۔ الا يعلمون كيف قال الله يا عيسٰى انّى متوفّيك۔ وقال فلمّا توفّيتنى فما يقبلون بعد كتاب مبين۔ الا يذ كرون ان اجماع الصحابة قد انعقد علٰى موت الانبياء كلّهم اجمعين۔ ايرتابون فيه اوكانوا من المعتدين۔ مالهم لا يذ كرون يومًا مات فيه رسُول الله وثبت معنى التوفّى بموته وجمع فى الصحابة كرب الاوّلين والاٰخرين۔ ونزلت عليهم مصيبة لن ينال كمثله احدمن العالمين۔ وقال بعضهم لا نسلم موت رسُول الله وانه سيرجع لقتل المنافقين۔ فحينئذ قام منهم عبد كان اعلم بكتاب الله وايّده الله بروحه فصارمن المتيقظين۔ وقال ايّها الناس ان محمدًا مات كمامات اخوانه من النّبيّين من قبله فلا تصرّوا علٰى ما تعلمون ولا تكونوا من المسرفين۔وقرء الاٰيةوقال وَمَامُحَمَّدٌ اِلَّا رَسُوْلٌ ۚ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ ؕ اَفَاۡئِنْ مَّاتَ اَوْ قُتِلَ انْقَلَبْتُمْ عَلٰٓى اَعْقَابِكُمْ ؕ وَ مَنْ يَّنْقَلِبْ عَلٰى عَقِبَيْهِ فَلَنْ يَّضُرَّ اللّٰهَ شَيْـًٔا ؕ وَ سَيَجْزِى اللّٰهُ الشّٰكِرِيْنَ [36] فما كان من الصحابة من خالفه اوتصدى للجدال كالمنكرين۔ ورُفع النزاع الذى نَشَأ بين الصحابة وقاموا من المجلس معترفين باكين۔ ولا يخفى انّ مقصود الصديق رضى الله عنه من قراءة هٰذه الاٰية ما كان الّا تعميم الموت وتسكين القلوب المضطرة بعموم هٰذه السنة و تنجية المحزونين ممّا نزل عليهم و تسلية المُضطرين۔ وافحام المنافقين الضاحكين۔ ولو فرضنا ان الاٰية تدل علٰى موت زمرة من الانبياء فقط لا على موت سائر النبيين فيفوت المقصود الذى تحرّاه الصديق بقراءة هٰذه الاٰية كما لا يخفى على العالمين ۔ فان ابابكر رضى الله عنه ما كان مقصده من قرأتها الا ان يبطل ما زعم عمرومن معه من حيات نبيّنا صلّى الله عليه وسلم وعوده الى الدنيا مرة اخرىٰ ولا يحصل هٰذا المقصود من هٰذه الاٰية التى قرء ت إستدلالا الّا بعد ان تُجعل الاٰية دليلًا وبُرهانًا علٰى مَوتِ جميع الانبياء الماضين۔ وليس يخفى ان مقصد ابى بكر من قراءة هذه الاٰية كان تسلية الصحابة بتعميم سنة الموت وتبكيت المنافقين۔ وازالةّ ماأخذ الصحابة بموت نبيهم من قلق و كرب وضَجرٍ وبكاء وانين ۔ فلو كان مفهوم الاٰية مقصورا علٰى ذكرموت البعض وحيات البعض فباىّ غرض

[36] Aali ‘Imraan 3:145

قرأها ابوبكر فانها كانت تخالف ماقصده بهٰذا المعنى وما كانت قراءتها مفيدةً للسامعين۔ وما كان حاصلها الا ان يزيد قلق الصحابة ويزيد حُزنهم فوق ما أُحزنوا و يسحّ الاجاج على جرح المجروحين۔ فان رسولهم الذى كان احبّ الاشياء اليهم وكان جاء هم كالعهاد۔ وكانوا يرقبون اثمار بركاته رقبة اهلّة الاعياد۔ مات قبل اتمام آمالهم وقبل قلع المفسدين۔ واقيالهم بل مات قبل اهلاك الكاذبين الذين ادعوا النبوّة وثوّروا الفتن فى الارضين۔ فلو كان ابن مريم وغيره احياءً من غير ضرورةٍ ومات نبيّنا الذى كانت ضرورته لأُمّةٍ من غير ريبة وشُبهةٍ فاىُّ رُزءٍ كان اكبر من ذالك لهٰؤلاءِ المخلصين۔ و اىّ مصيبة كانت اصعب من هذه المصيبة لقوم فقدوا نبيهم خير النبيين فلذٰلك كانوا يرجون طول حيات النبى النبيل وما كان احد منهم يظنّ انه يموت بهٰذا الوقت وبهٰذا العمر القليل۔ ويرجع الى ربّه الجليل و يتركهم متألمين۔ فحسبوا موته فى غير اوانه ۔ وقبل قطع الشوك و ارواء بستانه۔ وقبل اجاحة مسيلمة الكذّاب واعوانه فاخذهم ماياُخذ اليتامى الصغار عند هلاك المتكفّلين۔ وهذا اٰخر ما اردنا فى هٰذا الباب

والحمدُ للهِ رَبّ العالمين

تمّت

المؤلّف

ميرزا غلام احمد عافاهُ اللهُ وَايّد

[Tafsiri]

Jueni, Mungu Awarehemuni, kwamba muhtasari wa maneno yetu haya ni kwamba ijima juu ya kifo cha Masihi Isa mwana wa Mariamu na Manabii wengine waliotumwa kabla ya Seyidna na Mtume wetu Mteule[saw] yathibitika na kuimarika kwa nususi mkataa za Hadithi na masimulizi sahihi ya kufululiza. Na kila mwenye elimu ya Hadithi anajua kwamba ijima hii ilifanyika katika hadhara kubwa na hafla iliyohudhuriwa na watu

wengi wakati wa mkusanyiko wa Masahaba wakubwa na labibu. Basi, hawakujibidiisha kukanusha na kukataa rai ya Imamu wao mteule, hawakutaja kukosea kwake, wala hawakumshambulia, bali ikatulia mioyo yao alipotoa Siddik maelezo, na vita zao zilielekea kwenye amani na wakapata ushahidi madhubuti na hoja imara adhimu na wakaepukana na ubishi; na roho zikatakatika na mioyo ikang'arika na unyonge wao ukageuka kuwa nguvu. Na hapo kabla walikuwa lengo la Moto, au kama mtu aliyechomwa sana na njaa, kwa sababu ya kushindwa na subira yao kwa kifo cha mwongozi wao Nabii Mteule Muhammad[saw] na kwa kuhuzunika mioyo yao, na mioyo yao ikawa mitupu kwa kufariki mpendwa wao, mbora wa mahuluku, na wakawa kama waliokanganyikiwa. Basi alipoinuka mja wa Mungu, Abu Bakr Siddik[ra], akawafungulia mlango wa utambuzi na kawaonyesha kinywaji kitamu sana, na jambo likaamuliwa na wasiwasi wote ukaondolewa na sauti zikatulia. Na ijima ikafanyika juu ya kifo cha Masihi[as] na Manabii wote wa zamani. Bali hii ilikuwa ni ijima ya kwanza ya Masahaba baada ya kifo cha Khatamun-Nabiyyin. Na ijima hii ina shani kubwa kuliko ijima iliyofanyika juu ya ukhalifa wa Abu Bakr Siddik[ra]. Bila shaka Mashaba wote wakaafikiana juu yake na halikubaki kundi lolote. Wakakubali jambo lile bila kusita na kungoja kidogo, bali kwa utii na yakini kamili. Na wote walikuwa wakisoma aya hiyo na kukiri

kifo cha Mitume wote na kulia kwa kifo cha mkuu wa Mitume wote, mpaka Umar Faruk[ra] aliposikia aya ile akasema nikapigwa na bumbuazi na miguu yangu ikashindwa kunibebea; na akwa kwa huzuni kama majununi. Na Hassaan[ra] akasema katika wimbo wa huzuni juu ya kifo cha Mtume[saw] wa Mungu:

Yaani, Ee Seyidi wangu na habibu wagu, ulikuwa burudisho la macho yangu, basi kwa kifo chako nuru ya macho yangu imepotea, na sasa baada yako, sijali kwamba Isa au Musa au Nabii mwingine afe, kwani nilikuhofia wewe tu; na ulipokufa, basi na afe yeyote aliyekuwa miongoni mwa wa zamani. Na humo mnaashiria kwamba aya aliyosoma Abu Bakr Siddik[ra] ikawatanabahisha Masahaba wote kuhusu kifo cha Manabii wote. Basi, haikubakia ghamu yao kuwahusu hao wala hawakuwa wawahuzunikiao. Basi wakafurahia kifo cha wote baada ya kifo cha Mtume wao Mwaminifu[saw]. Na kama jambo lingekuwa kinyume chake, yaani kama ungethibitika uzima wa mmojawapo wa Manabii wa zamani kwa nususi ya Kurani na kwa aya za Furkani, basi huenda wangekufa wakimhuzunikia Mtume wao na huenda wangeungana na wafu. Lakini, walipojua kwamba Mtume wetu[saw] si wa pekee kufikiwa na kifo kutoka kwa Mungu Mjuzi, bali Manabii wote walifariki hapo kabla na wakanywa kikombe cha mauti, nyuso zao zikaangaza na mioyo yao ikafurahia. Basi,

wakasoma aya hii katika mitaa ya Madina na masokoni; na wanafiki wakajifia na hawakupata nafasi ya kupinga Islam kwa kifo cha Nabii wetu jamili na uzima wa Masihi, twamhimidi Mungu kwa msaada huu wazi. Neno la Islam lipo juu, na nuru yake inaangaza kila upande na kila ukingo. Mungu ndiye Aliyetuma Muhammad[saw] na Atamheshimu mpaka siku ya Kiama. Na ijima ilipothibitika hakikubaki kificho na asubuhi imeeneza nuru na mwale wa mwanga umetowesha giza. Basi, waulize wakanushi, je umebaki udhuru wowote. Haki bayana imebainika, na uthibitisho umekaririwa, na mbavu zimeimarika, na maradui na usingizi vimemalizika. Basi, anayedai baada yake kuondoa ijima hii na kulinasibisha jambo letu kuwa uzushi, basi anawajibika kuleta hoja mkataa kutoka katika Kitabu na Suna, na kuthibitisha ijima iliyofanyka juu ya uhai wa Masihi[as] katika zama za Masahaba. Na wataiwezaje hata wajifie kutafakari. Watawezaje ilhali hawanayo dalili kutoka kwa Mwenyezi Mungu wala hawana hoja bayana. Wanawafuata mababa zao waliokuwa wenyewe wakosefu. Mioyo yao imekuwa migumu na uaminifu umetoweka na sasa hawana la kufanya isipokuwa kupayuka, na hakuna kati yao yeyote atafutaye kama wamchao Mungu. Na wanapoambiwa, mwaminini aliyewafikieni kutoka kwa Mola wenu mwanzoni mwa karni na wakati wa haja iliyosikia mioyo ya waaminio,

husema hatumtambui aliyekuja na twamwona yu mmojawapo miongoni mwa madajali, ilihali walifundishwa kwamba atawafikia akiwa mwamuzi mwadilifu na ataamua baina yao katika mambo waliyohitilafiana. Basi, hakimu wao atawezaje kuwa mwenye kutiiwa na atakubalije kila la kipuuzi waliloafikiana. Wamekuwaje, hawatafakari kama wenye akili. Wananitusi kwa uadui bila elimu. Basi, Mungu ndiye Mbora wa kuhesabu na Hujua yaliyomo vifuani mwa walimwengu wote. Na hapo kabla walikuwa wakiomba ushindi na kufanya hesabu ya karne. Basi, alipowafikia waliomngojea wakatupilia mbali maagizo ya Mungu na Mtume[saw] wake nyuma ya migongo yao, kana kwamba amekuja katika wakati usio wake, na kana kwamba hawakumtambua kwa alama yoyote na wakawa miongoni mwa mwenye udhuru. Je hawakuona jinsi Mwenyezi Mungu Anavyotimiza kwa njia yake hoja kwa ishara za mbinguni na kulinda heshima ya Mtume[saw] wake na watu makafiri; bali wakamkataa na kusema yu mwasi na miongoni mwa wazushi. Basi, karibuni watajua kwamba nani ameasi na nani akamzushia Mungu uongo. Na kwa Mwenyezi Mungu haifichiki siri yoyote, na Mwenyezi Mungu Huwajalia mwisho mwema wamchao Mungu. Na sikuambiwa ila tu waliyoambiwa Mitume hapo kabla. Mioyo yao inafanana, na wamepambiwa amali zao, nao wanadhani

kwamba watapewa thawabu kwa kuniudhi, na wataingia Peponi kwa kunihakirisha, kukadhibisha na kuvunja heshima. Wakanikufurisha na kuniita mwasi na kunikadhibisha na kuniita jahili, na wakasema yu kafiri mbaya kuliko watu wote. Na kama Mungu Angetaka hawangesema hayo; lakini wakasema ili yatimie yalyomo katika Hadithi ya Mbora wa Mitume[saw]. Na hawasemi isipokuwa kujivunia na kujionyesha kwa watu, wala hawatafakari kama waadilifu wala hutakuta nyono zao zinatekeleza haki kama watu wema, bali utawakuta wengi wao wanafanya kila hila kwa kuzima nuru ya Mungu kwa vinywa vyao wala hawaogopi, isipokuwa husoma Kurani ambayo ama haipiti zoloto zao au wakawa miongoni mwa wanaokengeuka. Je hawajui Alivyosema Mwenyezi Mungu يٰعِيْسٰٓى اِنِّيْ مُتَوَفِّيْكَ na Akasema فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِيْ , basi watakubali nini baada ya Kitabu kilicho wazi. Je hawakumbuki kwamba ijima ya Masahaba ilifanyika juu ya kifo cha Manabii wote? Je wana shaka humo au ndio miongoni mwa warukao mipaka. Wamekuwaje, hawakumbuki siku aliyofia Mtume[saw] wa Mungu na kuthibitika maana ya *Tawaffi* kuwa kifo chake na zikajumuika katika Masahba huzuri za wa mwanzo na wa mwisho; na msiba uliwashukia ambao mfano wake hataupata yeyote ulimwenguni. Na baadhi yao wakasema, hatukubali kifo cha Mtume[saw] wa Mungu na kwa yakini yeye atarejea kwa kuwaua wanafiki. Basi,

hapo mja wa Mungu mmoja wa miongoni mwao akainuka aliyekuwa mjuzi zaidi wa Kitabu cha Mungu, na Mungu Akamsaidia kwa roho Yake, na alikuwa miongoni mwa walio macho. Na akaema, Enyi watu, bila shaka Muhammad[saw] amefariki jinsi ndugu zake Manabii wengine wa kabl yake walivyofariki. Basi msisisitizie msiyoyaju wala msiwe miononi mwa wapitao mipaka. Na akasoma aya, akasema وَ مَا مُحَمَّدٌ اِلَّا رَسُوْلٌ ۚ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ ؕ اَفَاۡئِنْ مَّاتَ اَوْ قُتِلَ انْقَلَبْتُمْ عَلٰٓى اَعْقَابِكُمْ ؕ وَ مَنْ يَّنْقَلِبْ عَلٰى عَقِبَيْهِ فَلَنْ يَّضُرَّ اللّٰهَ شَيْـًٔا ؕ وَ سَيَجْزِى اللّٰهُ الشّٰكِرِيْنَ . Basi, hakuwa yeyote miongoni mwa Masahaba aliyempinga au kujitokeza kubishana naye kama wakanao. Na hitilafu ikaondolewa iliyozuka baina ya Masahaba na wakatoka kikaoni wakikiri na kulia. Na si siri kwamba kusudio la Abu Bakr Siddik[ra] kwa kusoma aya hii lilikuwa kuthibitisha kufa kwa wote na kufariji mioyo iliyosumbuka kwa kueleza kanuni ya kufa kwa wote, na kuwaokoa wenye huzuni katika waliyoyashukiwa, na kuwatuliza wahangaikao, na kufumba midomo ya wanafiki wachekao. Na tukichukulia kwamba aya hii inaeleza kifo cha kundi moja tu la Manabii, si kifo cha Manabii wote, hapo itapotea shabaha aliyokusudia Abu Bakr siddik[ra] kwa usomaji wa aya hii kama vile haikuwafichika kwa wenye elimu. Kwani, kusudio la Abu Bakr[ra] kwa kusoma aya hii lilikuwa tu kwamba abatilishe aliyoyadhania Umar[ra] na wenzake kuhusu Nabii wetu[saw] kuwa hai na kurejea

kwake duniani mara nyingine. Na kusudio hili halipatikani kwa aya hii iliyosomwa isipokuwa baada ya kufanya aya hii kuwa dalili na hoja juu ya kifo cha Manabii wote wa zamani. Na siyo siri kwamba kusudio la Abu Bakr[ra] kwa kusoma aya hii lilikuwa kuwatuliza Masahaba kwa kufahamisha suna ya kufa kwa wote na kuwasuta wanafiki na kuwaondolea Masahaba huzuni, ghamu, mateso, kilio na maombolezo vilivyowasibu kwa kifo cha Nabii wao[saw]. Na kama muradi wa aya ungekuwa kutaja kifo cha baadhi na uzima wa baadhi, basi kwa shabaha gani akaisoma Abu Bakr[ra]? Kwani ikimaanisha hii, basi hii ilikuwa kinyume cha aliyoyakusudia, wala usomaji wake haukuwa wenye kuwafaa wasikilizaji. Wala yasigekuwa matokeo yake ila kuzidisha udhia wa Masahaba na kuongeza huzuni yao zaidi ya huzuni waliyoisha pata na kutia chumvi juu ya jeraha za waliojeruhiwa. Kwani, Mtume wao waliyempenda kuliko vitu vyote na akawajia kama mvua za kwanza za majira ya kuchipua, na walikuwa wakingojea matudna ya baraka zake kama kungojea hilali za idi, lakini akafa kabla ya kitimia matamanio yao na kabla ya kuwang'olea mbali wafisadi na viongozi wao, bali akafariki kabla ya kuwaangamiza waongo waliojidai unabii na kuchochea fitina ardhini. Basi, kama mwana wa Mariamu na wengineo wangekuwa wazima bila kuhitajika, na Nabii[saw] wetu amekufa aliyehitajika

kwa umati huu bila wasiwasi wala shaka, basi kulikuwa na balaa gani kubwa iliyokuwa kuliko hii kwa hao wenye ikhlasi, na ulikuwa msiba gani mzito zaidi kuliko msiba huu kwa watu waliofiwa na Nabii[saw] wao Mbora wa Manabii. Basi kwa hiyo walitarajia Nabii[saw] wao angeishi umri mrefu; na kulikuwa hamna hata mmoja aliyedhani miongoni mwao kwamba yeye atakufa wakati huo na katika umri huo mdogo, na atarejea kwa Mola wake Jalali na kuwaacha wakiumia. Kwa hiyo, wakafikiri kifo chake kimetokea kabla ya wakati wake na kabla ya kukata miba na kumwagilia bustani yake, na kabla ya kuangamiza Musailima kadhabu na wasaidiazi wake. Basi, wakapatwa na hali inayowapata mayatima wadogo wakati wa kifo cha wasimamizi wao. Na huu ni mwisho wa yale tuliyoyanuia katika somo hili. Na sifa zote njema zinamhusu Mungu Mola wa walimwengu.

**Tamati**

**Mwandishi**

**Mirza Ghulam Ahmad, Mwenyezi Mungu Amsamehe na kumsaidia**

☆